Nipashe
Jumatano Mei 13, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580230
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Waziri: Wadau wamekubali biashara ya utalii iendelee

UKURASA 3


Yanayowadhalilisha wanawake kwenye uchaguzi yakomeshwe
siasa
HABARI BORA NA KAMILIFU
Uchaguzi mkuu 2020 kinamama kubanwa na mifumo kandamizi?
BALOZI MAHIGA
Mbobezi wa UDSM aliyetumika UN kuleta amani maeneo korofi

UKURASA 13

# SERIKALI: SUKARI YAJA

**TANI** 4,000 zawasili bandarini, 21,000 ziko njiani, yaanika sababu za kuadimika kwake... *Endelea ukurasa 2*



Wakazi wa Mji wa Muheza, mkoani Tanga, wakiwa kwenye foleni ya kununua sukari kwenye moja ya maduka ya jumla jana, kutokana na kuadimika. **Picha ndogo:** Mkusanyiko wa baadhi ya wafanyabiashara wadogo wa Manispaa ya Morogoro, wakisubiri kuandikishwa majina kwa ajili ya kununua bidhaa hiyo, katika mtaa wa Nunge. **PICHA: STEVEN WILLIAM/FRANK KAUNDULA**

TISHIO LA CORONA

## Tanzania kuhifadhi akiba ya chakula tani 735,000

UKURASA 2

## BOT YALEGEZA MASHARTI MIKOPO

UKURASA 3

BAA LA CORONA



Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kujiweka 'fit' katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19 ni changamoto kwa watu wengi. Lakini ni muhimu kupanga kila siku njia za kukufanya uwe fit na kupunguza kukaa sehemu moja kwa muda mrefu. Tembea zaidi kuliko kukaa.

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

MICHEZO **AJIBU SI WAKUICHEZEA TENA YANGA- MENEJA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA




Baadhi ya malori yenye mizigo yaliyokuwa yakisafirisha kuelekea Zambia, yakiwa yameegeshwa katika eneo la Tunduma, mkoani Songwe jana, baada ya nchi hiyo, kufunga mpaka wake. Habari Uk. 3. **PICHA: MANUEL KAMINYOGE**

# Serikali: Sukari yaja

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

SERIKALI, imewatoa hofu Watanzania kuhusu upatikanaji wa sukari nchini, akibainisha kuwa tayari tani 4,000 za sukari zimeshawasili kwenye Bandari ya Dar es Salaam na shehena ya tani 21,000 inatarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi huu.

Vilevile, serikali kupitia kwa Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, imetaja sababu tatu za kupungua kwa sukari nchini, ambazo ni pamoja na meli zilizokuwa zimebeba bidhaa hiyo kufaulisha mzigo katika meli zingine na kusababisha sukari iliyokuwa inaingia nchini kutokidhi mahitaji.

Waziri hasunga aliyasema hayo bungeni jijini hapa jana, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 229.84.

Hasunga alisema kulipuka kwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona duniani, nako kumechangia kuchelewa kwa bidhaa hiyo kufika kwa wakati nchini, lakini akasisitiza kuwa Watanzania hawapaswi kuwa na hofu kwa kuwa tani nyingi za sukari zimeshawasili.

Waziri huyo alibainisha kuwa kuanzia Mei 10 hadi jana, kiasi cha sukari kilichokuwa kimewasili kwenye Bandari ya Dar es Salaam, ni tani 4,000 na kwamba tani 21,000 ziko njiani na zinatarajiwa kuwasili nchini mwishoni mwa mwezi huu.

Alisema tani zingine 500 kutoka Afrika Kusini, zimeshawasili katika Bandari ya Kasumuru, hivyo uhaba wa sukari uliopo nchini kwa sasa, utamalizika hivi karibuni.

"Mahitaji ya sukari nchini ni tani 35,000 kwa mwezi, hivyo zilivyoingizwa tani 40,000, waliamini zitatosha maana viwanda vilikuwa vianze uzalishaji Mei.

"Hata hivyo, kutokana na mvua kuendelea kunyesha ni kiwanda kimoja tu kimeonyesha dalili ya kuanza uzalishaji mwisho wa mwezi.

"Niwahakikishie Watanzania kwamba, sukari iliyoingia na hatua zilizochukuliwa, inatosha kabisa na hatuhitaji kuwa na upungufu wa sukari," Waziri alifafanua.

Kiongozi huyo wa serikali alitaja sababu nyingine ya kuchelewa kuingia kwa sukari nchini kuwa ni mlipuko wa virusi vya corona duniani pamoja na baadhi ya wafanyabiashara kuficha sukari kwa lengo la kufanya ulanguzi.

"Wizara kupitia Bodi ya Sukari, ilifanya uchunguzi wa kina na kwa kutumia Sheria ya Tasnia ya Sukari, ilichukua hatua ya kutangaza bei elekezi ya jumla na rejareja katika mikoa yote ya Tanzania Bara kwa lengo la kukabiliana na wafanyabiashara wasio waaminifu.

"Sasa hivi, ni kweli katika maeneo mbalimblai kuna upungufu wa sukari. Ni kutokana na meli nyingi zimekuwa zikifaulisha kwenye meli nyingine na kusababisha sukari kutokuja kwa wakati unaotakiwa.

"Niwaombe wenzangu wanaohusika, wahakikishe sukari iliyofika bandarini, wanaitoa na kusimamia usambazaji katika mikoa yote nchini," aliagiza.

Hasunga alisema serikali ilikokotoa gharama ya bei ya sukari inayotoka nje hadi inapofika nchini na kubaini ni Dola za Marekani 350 hadi 500 kwa nchi za mbalimbali kama vile Brazil.

Alisema walipokokotoa kwa bei ya Tanzania, walibaini sukari haitakiwi kuzidi bei elekezi iliyotangazwa na serikali.

## Tanzania kuhifadhi akiba ya chakula tani 735,000

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema katika kukabiliana na athari za ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona, serikali inatarajia kununua chakula tani 735,000.

Aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Hasunga alisema mlipuko wa ugonjwa wa ugonjwa huo umeathiri sekta mbalimbali za kiuchumi nchini ikiwamo sekta ndogo ya mazao.

Alisema ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na ugonjwa huo wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), itanunua tani 65,000 kutokana na fedha zilizotengwa kwenye bajeti 2019/2020 Sh. bilioni 15 na fedha za mapato ya ndani Sh. bilioni 24, ili kuongeza hifadhi ya chakula kufikia tani 103,698.794 ambayo inajumuisha akiba ya tani 38,698.794.

"Mahitaji ya nafaka kwa mwezi kwa Watanzania wote ni wastani wa tani 750,000. Tukichukulia asilimia 20 ya Watanzania ndiyo pekee watakaohitaji kununua chakula kwa asilimia 100 ambao mahitaji yao ya nafaka kwa mwezi yatakuwa tani 145,000.

"Kiasi hicho cha chakula ni kidogo endapo dharura ya mahitaji ya chakula yatatokea. Hivyo, katika kukabiliana na upungufu huo, Wizara kupitia NFRA itanunua tani 435,000 zenye thamani ya Sh. bilioni 217.5, ambazo zitatosheleza kwa miezi mitatu," alisema.

Waziri Hasunga alibainisha kuwa, kuanzia Julai mwaka huu, NFRA itanunua tani 300,000 kupitia bajeti iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na mapato ya wakala. Hivyo kufanya jumla ya chakula kitakachonunuliwa kuwa tani 735,000.

Alisema Wizara ya Kilimo imefanya tathmini na kubaini kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2019/2020 haujaathiriwa na mlipuko wa virusi vya corona kwa kuwa pembejeo zilikuwa zimeshawasili nchini.

Lakini, katika kukabiliana na uhaba wa mbolea unaoweza kutokea kutokana na kuendelea kuwapo kwa tatizo la ugonjwa wa corona, Hasunga alisema wizara itaruhusu mbolea kuingizwa nchini bila kufuata utaratibu wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja.

Waziri huyo alisema mlipuko wa virusi hivyo pia haujaathiri mazao ya asili ya biashara ambayo ni pamba, korosho na kahawa kwa kuwa misimu yake ya mauzo iliishia Machi mwaka huu.

"Kwa zao la tumbaku wakulima wameshafunga mikataba na wanunuzi kwa ajili ya msimu wa 2020/21. Mazao ambayo yameonesha dalili za kuathirika ni chai na mazao ya bustani ambayo masoko na usafirishaji wake nje ya nchi umeathirika," alisema.

Waziri huyo pia alibainisha kuwa, katika kipindi cha miaka mitano, Pato la Taifa linalotokana na kilimo kwa kutumia bei za mwaka 2015, limeongezeka kwa asilimia 17 kutoka Sh. trilioni 25.2 mwaka 2015 hadi Sh. trilioni 29.5 mwaka 2019.

Alisema sekta ya kilimo imeendelea kutoa ajira kwa Watanzania kwa asilimia 58 mwaka 2018, imechangia asilimia 28.2 ya Pato la Taifa ambapo sekta ndogo ya mazao imechangia asilimia 16.2.

Alisema hiyo imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo vyakula vinavyotokana na mazao ya kilimo.

Alisema kati ya mwaka 2015 hadi 2019, sekta ya kilimo imeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.2 na kwamba sekta ndogo ya mazao imeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.8.

Hasunga aliyataja maeneo yaliyopewa kipaumbele katika mwaka ujao wa fedha kuwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Progamu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II); kuboresha mifumo ya kitaasisi, bodi na sheria za kilimo kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya mazao ya kilimo na kuunganisha wakulima wadogo na mashamba makubwa ili kuendeleza kilimo cha kibiashara, kupata ujuzi na maarifa ya kilimo chenye tija.

Kurahisisha upatikanaji wa huduma za pembejeo na masoko; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, maghala, masoko na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo; na kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za mazao na upatikanaji wa pembejeo nyingine za kilimo na kuzisambaza kwa wakulima.

Aliyataja maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele kuwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya ushirika pamoja na kuweka mifumo itakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wanaushirika na wadau wengine wa sekta ya kilimo.

Pia, kuongeza matumizi ya teknolojia bora katika uzalishaji wa mazao na tija; kuimarisha vituo vya utafiti, vyuo vya mafunzo na vituo vya mafunzo kwa wakulima kwa kujenga miundombinu wezeshi na kuboresha maarifa na ujuzi kwa watafiti, wakufunzi na wazalishaji kwa lengo kukuza kilimo; kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa udongo kuendana na mahitaji ya mazao ya kilimo kimaeneo; na kuimarisha masuala mtambuka katika kilimo.

***SOMA HOTUBA YA WAZIRI HASUNGA UK. 7-11**

## HABARI KITAIFA

# Wadau utalii wakubali kufungua biashara

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, amesema kuwa wadau wa utalii nchini wamekubaliana kufungua biashara huku wakichukua tahadhari zote.

Uamuzi huo umekuja siku chache baada ya kikao baina ya wadau na serikali kujadili namna ya kufungua biashara ifikapo Juni, mwaka huu.

Katika ukurasa wake wa Tweeter, Waziri huyo alieleza hatua zilizochukuliwa ni kuhakikisha wageni wanaendelea kuingia nchini na kujilinda kwa kiasi kikubwa dhidi ya janga hilo.

"Kikao chetu na wadau wa utalii kimeenda vizuri sana. Sekretarieti inakamilisha taarifa, kutakuwa na protokali ya mapokezi, chombo cha usafiri, chumba n.k. Tumekubaliana kimsingi tufungue biashara ya utalii kwa kuweka tahadhari zote za kuzuia maambukizo ya corona," alisema.

Mei 7, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2020/21, alisema ni lazima watu wajifunze kuishi na corona ikiwa ni pamoja na kuondoa ulazima wa wageni kujitenga kwa siku 14.

Alisema ombi jingine lililowasilishwa ni kufungua mipaka kwa kuruhusu ndege za kimataifa kutua nchini, huku akitaja mashirika ya ndege makubwa duniani ambayo yameanza safari zake kuwa ni KLM, Emirates na Swiss.

Vile vile, alieleza jinsi corona ilivyoathiri sekta hiyo kwa mashirika likiwamo Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Tawa).

Mwaka huu Tanapa ililenga kukusanya jumla ya Sh. bilioni 363.9, lakini itakusanya Sh. bilioni 64 au chini ya hapo, huku Ngorongoro, ilikadiria kukusanya Sh. bilioni 162.7, lakini itakusanya Sh. bilioni 58.

Alisema TFS ilikadiria Sh. bilioni 153.6, lakini zitakusanywa Sh. bilioni 121 huku Tawa ilikadiria Sh. bilioni 58.1, sasa itakusanya Sh. bilioni 22.

Waziri huyo alisema mapato yanayotokana na utalii yatashuka kutoka Sh. trilioni 2.6 zilizotarajiwa hadi kufikia Sh. milioni 598.

Kwa upande wa ajira zitapungua kutoka 623,000 hadi kufikia 146,000, idadi ya watalii itashuka kutoka 1,867,000 waliotarajiwa hadi kufikia 437,000.



Msimamizi wa kampuni ya ujenzi ya CCECC, Saidi Mbua (kulia) na mafundi wenzake, wakiendelea na kazi ya ujenzi wa barabara zitakazounganisha daraja la juu la Ubungo (Ubungo Interchange), katika Barabara ya Sam Nujoma, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# BoT yatangaza ahueni mikopo benki

**Na Enock Charles**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imetangaza hatua sita za kisera zilizochukuliwa kukabiliana na athari za corona kwenye benki nchini, ikiwamo kupunguza riba, amana, hati fungani na dhamana.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana, uamuzi huo umefikiwa na kamati ya sera ya fedha ya Bodi ya BoT na kutoa ahueni kwa taasisi za fedha.

Ilibainisha kuwa lengo la hatua hizo ni kudumisha uthabiti wa sekta ya fedha na upatikanaji wa huduma za fedha nchini.

Hatua zilizochukuliwa ni kushusha kiwango cha chini cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa BoT kutoka asilimia saba hadi sita, kuanzia Juni 8, mwaka huu.

Kuongeza unafuu kwenye dhamana na hati fungani za serikali zinazotumika na benki kwa kupunguza kiwango cha dhamana kutoka asilimia 10 hadi tano kwa dhamana za muda mfupi na kutoka asilimia 40 hadi 20 kwa hati fungani kuanzia Mei 12, mwaka huu.

Nyingine ni kushusha kiwango cha riba kwa benki kukopa BoT kutoka asilimia saba hadi tano, kuanzia jana ili kuwezesha kuongeza wigo wa benki kukopa kutoka BoT kwa riba nafuu na hivyo kupunguza riba ya mikopo kwa wateja.

Vile vile, BoT imezitaka benki na taasisi za fedha kutathmini athari za mlipuko wa virusi vya corona kwenye urejeshaji wa mikopo kujadiliana na wakopaji namna ya kurejesha mikopo yao na kwamba Benki Kuu itatoa unafuu kwa benki zitakazofanya hivyo.

Nyingine ni kuendelea kufanya tathmini ya athari za mlipuko ya ugonjwa wa homa ya virusi vya corona katika sekta mbalimbali za uchumi na kuchukua hatua stahiki ili kupunguza madhara ya athari hizo.

# Magari 1,000 yakwama mpaka wa Tunduma

**Na Manuel Kaminyoge , SONGWE.**

ZAIDI ya magari 1000 yanayosafirisha mizigo kwa kupitia mpaka wa Tunduma kuelekea Zambia yameshindwa kuvuka mpakani kutokana na hatua iliyochukuliwa na serikali ya nchi hiyo ya kufunga mipaka kwa muda usiojulikana kukabiliana na virusi vya corona.

Ikiwa ni siku ya pili tangu serikali ya Zambia kufunga mpaka, shughuli zote za mpakani zimesimama, hali iliyosababisha magari yaliyobeba mizigo kama chakula na mafuta kukwama kuendelea na safari .

Brigedia Jeneral Nicodemas Mwangela, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, jana alifika katika mpaka huo uliopo mji wa Tunduma, wilaya ya Momba, ambapo alijionea bidhaa mbalimbali zikiwa zimekwama kuvuka.

Aliwataka wasafirishaji mizigo hiyo kuwa na subira ambapo alisema kuna mazungumzo yanaendelea, na kwamba huenda mpaka huo ukafunguliwa mapema kufuatia makubaliano ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuzuia kufunga mipaka kabisa badala yake bidhaa muhimu kama mafuta na chakula viruhusiwe kuvuka.

Aidha, liwataka wasafirilishaji kuondoa hofu kutokana naadhabu ambazo wanaweza kukumbana nazo kufuatia sheria ya kutokaa mpakani bila kuvuka kwa zaidi ya siku saba.

"Tunduma ni salama, Songwe ni salama hakuna haja ya wananchi kuwa na hofu, endeleeni kuchapa kazi," alisema mkuu wa mkoa.

Juzi, serikali ya Zambia ilianza utekelezaji wa agizo hilo kwa kufunga mageti yote mawili ya kuingilia nchini humu pamoja na maduka, na shughuli zote zinazofanywa kwenye eneo la mpaka, hali iliyoibua vilio kwa wafanyabiashara wa mji wa Tunduma.

Wakizungumza baada ya utekelezaji wa agizo la kufunga mpaka, wafanyabiashara hao walisema kwa sasa wana mazingira magumu ya kumudu maisha yao kwani maisha ya mji wa Tunduma yanategemea sana biashara.

Neema Kalinga, mmoja wa wafanyabiashara waliofungiwa maduka, alisema hawana cha kufanya kwani walishindwa hata kuchukua chochote dukani kufuatia askari wa Zambia kufunga maduka yote majira ya alfajiri, na kwamba hakukutolewa taarifa yoyote kwa ajili ya kujiandaa na hatua hiyo.

Aliongeza serikali ya Zambia ilipaswa kutoa angalau siku moja kwa ajili ya wafanyabiashara kujiandaa kwani wangeweza hata kuhamisha bidhaa zo ili mpaka ukifungwa maisha mengine yaendelee.

George Kyando, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, alisema ulinzi mpakani umeimarishwa vya kutosha, na Watanzania waendelee na shughuli zao kama kawaida.

# Msajili awasubiri wabunge waliofukuzwa na Chadema

**Na Enock Charles**

MSAJILI wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, amesema hawezi kuingilia suala la wabunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kufukuzwa uanachama wa chama hicho hadi pale atakapopelekewa malalamiko.

Akizungumza kwa simu na Nipashe, Jaji Mutungi alisema kila taasisi ina taratibu zake, na kwamba atakapopelekewa malalamiko ataangalia kama kuna uvunjifu wa sheria za nchi katika suala husika.

"Wahusika (wabunge) hawajaja kwetu kulalamika kwa hiyo wao wanaheshimu taratibu za chama chao, wakija tutaingilia hilo suala," alisema Jaji Mutungi.

Juzi, saa chache baada ya Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, kutangaza uamuzi wa kuwatimua wabunge hao, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alimuomba msajili wa vyama vya siasa kukiangalia chama hicho kikuu cha upinzani na namna kinavyoendeshwa kwa madai kuwa kinafanya maamuzi ya kibabe dhidi ya wabunge wake.

Wabunge waliofukuzwa kwa makosa ya utovu wa nidhamu ni Mbunge wa Momba, David Silinde, Mbunge wa Moshi Vijijini, Anthony Komu, Mbunge wa Rombo, Joseph Selasini na Mbunge wa Bukoba Mjini, Wilfred Lwakatare.

Aidha, waliotakiwa na Kamati Kuu ya Chadema kujieleza ni wabunge wa viti maalum Suzan Masele, Joyce Sokombi, Rose Kamili, Latifa Chande, Lucy Mlowe, Sware Semesi, Sabrina Sungura na Anne Gideria.

Wengine ni Mbunge wa Moshi Mjini, Jaffary Michael, Mbunge wa Kilombero, Peter Lijualikali na Mbunge wa Karatu William Kambalo.

Wabunge hao walichukuliwa hatua hiyo kwa madai ya kukaidi maelekezo ya chama ya kutohudhuria vikao vya Bunge, ikiwa ni sehemu ya tahadhari dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona.




Rais wa Klabu ya Rotary ya Mbezi Beach, Guru Sykes (kushoto), akikabidhi vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi vya wa corona kwa mwenyekiti wa waendesha bajaji na pikipiki wa kituo cha Africana, Damiani Elias, kwa ajili ya matumizi ya kujikinga, jijini Dar es Salaam jana. Zaidi ya waendesha bajaji na pikipiki 300, wamenufaika kwa kupata vifaa hivyo. Katikati ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mbezi Beach 'B', Asha Voniatis. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kortini tuhuma utakatishaji mil. 383/-

**Na Hellen Mwango**

MKAZI wa Goba jijini Dar es Salaam, Edgael Lema (43), amefikishwa mahakamani kujibu mashitaka nane yakiwamo kukutwa na mazao ya misitu, magogo na kutakatisha zaidi ya Sh. milioni 383.

Mshitakiwa huyo alisomewa mashitaka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Vicky Mwaikambo.

Wakili wa Serikali Mwamdamizi, Maternus Marandu, alidai mshitakiwa huyo anakabiliwa na mashitaka ya kuongoza genge la uhalifu, kusafirisha magogo, kughushi, kutoa nyaraka za uongo, kukwepa kodi na kutakatisha fedha.

Ilidaiwa katika shitaka la kwanza kati ya Novemba 2015 na Januari 2016 mahali pasipofahamika nchini, mshitakiwa akiwa na watu wengine ambao hawapo mahakamani, walijipanga kuongoza genge la uhalifu huku wakijua kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Shitaka la pili, ilidaiwa kati ya Novemba 2015 na Januari 2016 mahali tofauti jijini Dar es Salaam, mshitakiwa akiwa na watu wengine ambao hawapo mahakamani, walisafirisha kontena 18 zenye mazao ya misitu ikiwamo vipande vya magogo 5,296 aina ya mkurungu yenye thamani ya Sh. 383,140, 840, mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Maliasili.

Katika shitaka la tatu na la nne la kugushi Kati ya Mei 14 mwaka 2015 na Machi 16 mwaka 2015 eneo lisilojulikana nchini, mshitakiwa akiwa na watu wengine ambao hawapo mahakamani, walitengeneza nyaraka za uongo wakijaribu kuonyesha kuwa imetolewa na ofisi ya Serikali ya Zambia, huku wakijua si kweli.

Katika shitaka la tano na sita, tarehe isiyojulikana eneo la Makao Makuu ya Bandari ya Dar es Salaam, mshitakiwa akiwa na watu wengine ambao hawapo mahakamani huku wakijua ni udanganyifu walitoa nyaraka za uongo kwenye ofisi hiyo wakionyesha nyaraka hizo zimetolewa na ofisi ya Serikali ya Zambia, huku wakijua si kweli..

Shitaka la saba kati ya Novemba 2015 na Januari 2016 jijini Dar es Salaam, mshitakiwa akiwa na nia ya kukwepa kodi, alitoa nyaraka za uongo ili kukwepa kulipa kodi ya Sh. 383, 140, 840, huku akijua kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Shitaka la nane, ilidaiwa kati ya Novemba 2015 na Januari 2016 jijini Dar es Salaam, mshitakiwa alijipatia Sh. 383, 140, 840, huku akijua fedha hizo zilikuwa zimetokana na uhalifu wa kukwepa kulipa kodi.

Mshitakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu Mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

## UFUPI

### Wahoji mazungumzo kigogo Takukuru, DPP

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayomkabili Mkurugenzi wa zamani wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor, umedai mazungumzo ya kukiri makosa kati ya mshtakiwa huyo na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) yanaendelea.

Aidha, Jamhuri imedai mazungumzo yakikamilika wataijulisha mahakama hivyo unaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Madai hayo yalitolewa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu, kesi hiyo ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa baada ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Godfrey Isaya anayesikiliza usikilizwaji wa awali kuwa na udhuru.

Wakili wa Serikali, Kija Luzungana, alidai kesi imepangwa kwa ajili ya kutajwa upelelezi haujakamilika.

Hata hivyo, Wakili wa Utetezi, Elia Mwingira, alihoji kuwa kuna mazungumzo yanaendelea kati ya mshtakiwa na DPP walitegemea jana kupata taarifa ya muafaka wake.

Luzungana akijibu hoja ya utetezi alidai ofisi yao inataarifa ya mazungumzo hayo, lakini hayajakamilika, yakikamilika wataifahamisha mahakama.

Mshtakiwa huyo ambaye anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo mashtaka manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanyanyifu na kutakatisha Sh. bilioni 1.477 kuingia kwenye majadiliano na DPP, lakini wakashindwa kuelewana na majadiliano hayo yalikufa Januari, 2020 na baadaye mchakato ulianza upya.

### ACT sasa yataka takwimu za corona

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kutoa takwimu za hali ya maambukizo ya corona na vifo, ikiwa ni namna ya kuongeza kasi ya Watanzania kuchukua tahadhari.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Makamu Mwenyekiti Bara, Doroth Semu, zimepita siku 13 tangu serikali itoe takwimu za mwisho za maambukizo jambo ambalo halipaswi kuwa hivyo.

"Tangu Aprili 29 ndiyo tulipata taarifa mpya kuhusu wagonjwa walipona na watu waliopoteza maisha," alisema.

Aidha, chama hicho limetaka kuongezeka kwa mshikamano mkubwa baina ya serikali, vyama vya siasa, asasi zisizo za kiserikali na viongozi wa dini kukaa pamoja na kukubaliana njia ya kisayansi ya kupambana na janga hilo.

Semu alisema bado kuna mengi yanatakiwa kufanywa kama bajeti ya corona, kutegemea zaidi sayansi, kupima watu wengi na kwa wakati, kuhakikisha kuwa hakuna mikusanyiko, kutoa vifaa kinga kwa madaktari kwa wakati na vya kutosha.

HABARI KITAIFA

# Ummy awataka wauguzi tahadhari virusi corona

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imewataja wauguzi kuwa ni wapambanaji wakubwa katika utoaji huduma kwa washukiwa virusi vya corona, na kuwataka wazingatie tahadhari zote ili kutoruhusu maambukizi zaidi.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na watumishi wa Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani.

"Tufanye kazi kwa kuzingatia kwamba tuna mlipuko wa corona hivyo, ni lazima tuchukue tahadhari sisi wenyewe kama wauguzi kujikinga kwa kuzingatia kanuni na miongozo ya udhibiti wa maambukizo," alisema.

Pia aliwataka wafanya kazi wao kwa kuzingatia kanuni na miongozo ya utoaji huduma kwa wagonjwa na washukiwa na virusi vya corona.

Waziri Ummy alisema serikali itaendelea kutambua, kuheshimu na kuthamini kazi kubwa na nzuri zinazofanywa na kundi hilo.

"Katika jitihada za serikali za kuboresha huduma za uuguzi na ukunga wizara imekamilisha mwongozo wa utoaji huduma kwa kuzingatia utu, heshima na maadili," alisema.

Alisema hadi sasa jumla ya wauguzi 778 katika hospitali 15 za rufani za mikoa wamepata mafunzo kuhusu utoaji huduma kwa kuzingatia utu, heshima na maadili.

Alisema mafunzo hayo yataendelea kutolewa katika ngazi zote za kutolea huduma na wametengeneza mfumo wa kupokea taarifa, malalamiko na kero kutoka vituo vya kutolea huduma ili kusaidia ufuatiliaji na kuzitatua.

Waziri Ummy aliwataka wauguzi wafanye kazi zao kwa kuzingatia weledi na maadili ya huduma ya uuguzi.

Alisema licha ya Tanzania kuwa na wauguzi 30,451 bado kuna upungufu kwenye vituo vya afya na kwamba serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha ajira kwao.

"Rai yangu kwa wananchi endeleeni kutii maelekezo na maagizo ya serikali na ya wataalamu wa afya ili kuepuka kuenea kwa maambukizi na kuwapunguzia mzigo watoa huduma ambao wanajitoa," alisema.

Kwa upande wake, Rais wa Chama cha Wauguzi na Wakunga Tanzania (TANNA), Alexander Baluhya, alisema ili kuwapo kwa huduma bora na salama za afya, nchi inapaswa kuwa na wataalamu wenye weledi na mazingira bora ya kazi.

Alisema idadi hiyo ya wauguzi walioajiriwa nchini ni takribani asilimia 60 ya wataalamu wote wa afya.

"Wauguzi hawa wanatoa zaidi ya asilimia 80 ya huduma za afya ambazo zimekuwa zikitolewa kwa Watanzania. Hivyo upungufu wa wauguzi na wakunga ni asilimia 48," alisema.

Aidha, aliwapongeza wauguzi kwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili ya taaluma yao hasa katika kipindi hiki cha maambukizi ya virusi vya corona.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Zefrin Lubuva, akijaribu moja ya mashine 10 za kunawa mikono, zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 2.5, alizopokea msaada kutoka Taasisi ya Dk. Msuya, kwa ajili ya kutumika kwenye maeneo ya huduma za jamii wilayani humo jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Dk. Ombeni Msuya na Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Abdul Msuya. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Silaha kivita yanaswa msako wa majangili

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

JESHI la Polisi mkoani Arusha limekamata bunduki ya kivita aina ya AK 47 yenye namba za usajili H 49 na risasi 12 ndani ya magazini katika operesheni dhidi ya ujangili.

Vilevile, imeelezwa kuwa, katika tukio hilo, jeshi hilo pia limekamata watu wawili wanaodaiwa kujihusisha na ujangili, lakini majina yao yamehifadhiwa ili kutoharibu msako unaoendelea dhidi ya raia wa Kenya wanaotafutwa baada ya kufanikiwa kuwakimbia askari waliokuwa wanawasaka.

Akizungumza jana jijini Arusha, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema bunduki hiyo ilikamatwa Mei 10 mwaka majira ya saa saba mchana katika Kitongoji cha Oloshoo, Kijiji na Kata ya Enguserosambu, Tarafa ya Loliondo wilayani Ngorongoro.

Alisema bunduki hiyo ilipatikana baada ya kikosi kazi kupata taarifa ya siri kuwa kuna watu wanne, wawili ni Watanzania na wengine raia wa Kenya, wameonekana maeneo ya mpakani wakipanga kwenda kuwinda wanyama katika moja ya mbuga muhimu nchini.

"Baada ya kupata taarifa hizi, kikosi kazi chenye askari machachari, wazalendo na wenye weledi wa hali ya juu, kiliendelea na uchunguzi wa kina ili kubaini ukweli wa taarifa hizo," alisema.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alisema kuwa, baada ya uchunguzi, walifanikiwa kuinasa bunduki hiyo na risasi zake zikiwa mikononi mwa watuhumiwa wawili ambao ni Watanzania na wenzao wawili, raia wa Kenya walikimbia.

Kamanda Shana aliwataka watuhumiwa waliokimbia kujisalimisha mara moja katika kituo chochote cha polisi, vinginevyo watalazimika kutumia nguvu kubwa kuwatafuta.

Alisema katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya corona, ni vyema wahalifu wakafahamu jeshi hilo halijalala wala halijajifungia kwenye nyumba, bali linaendelea na kazi na yoyote anayejaribu kufanya uhalifu, hatakuwa salama.

"Ninawashukuru wananchi wote wanaoendelea kutoa ushirikiano kwetu, ili kuwakamata wahalifu na endeleeni kufichua wahalifu wanaojihusisha na uwindaji haramu, ujambazi na uhalifu wowote na donge nono tutalitoa kwa mfichua siri," alisifu.

## Wakulima tumbaku kupimwa corona kabla mauzo kudhibiti

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

KAMPUNI zitakazonunua tumbaku msimu huu, zimeagizwa kuwa na kifaa cha kupima joto wakulima pamoja na kuwaruhusu miongoni mwao kuwawakilisha wenzao kuleta mauzo, hatua itakayosaidia kudhibiti maambukizo mapya ya virusi vya corona.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku Tanzania, Stanley Mnozya, alisema agizo hilo limo katika mwongozo wa ununuzi wa zao hilo kwa msimu wa mwaka huu, ambao wameuandaa na kuusambaza kwa wadau pamoja na Wizara ya Kilimo, waujadili.

Akiongea na Nipashe, Mnozya alisema kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu katika kuepusha mikusanyiko, wameandaa mwongozo huo ili kudhibiti maambukizo mapya ya virusi vya corona vinavyosababisha maradhi ya homa kali ya mapafu (Covid-19), ambavyo vimeitikisa dunia.

"Ieleweke kuwa mwongozo huu si msahafu unaweza kubadilika kutokana na matakwa ya wadau ama wizara, lakini kwa mauzo ya awali tunauzingatia," alisema Mnozya.

Mnozya alisema pia katika soko la msimu huu, watahakikisha wanatunza kumbukumbu nzuri ya wote watakaohusika katika soko la siku hiyo ili ikitokea miongoni mwao kubainika ana maambukizo kuwa rahisi kuwapata na kufuata kanuni za afya kwa wote waliohusika na soko la siku hiyo.

Mnozya alisema zao hilo ambalo msimu uliopita liliingiza Sh. bilioni 232 kwa kilo milioni 71, huku kukiwa na kilo milioni 14, zilizokuwa nje ya mkataba.

Hata hivyo, alisema zilinunuliwa na kampuni za wazawa na mkataba wa msimu huu ni kuzalisha kilo milioni 57, umeanza masoko yake rasmi Mei 11, mwaka huu.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika (KACU), Emmanuel Charahani, alisema soko hilo msimu huu limechelewa kwa kutoa fursa kwa wadau wa zao hilo kukutana kujadili njia sahihi ya kufanyika biashara hiyo bila kuathiri wakulima kupata maambukizo ya virusi vya corona.

Charahani alitoa wito kwa wakulima kutoziangusha kampuni za wazawa ambazo msimu huu zimejitokeza kununua zao hilo, kwa kupanga vyema tumbaku yao katika madaraja yanayostahili ili kutoondoa ubora wake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sheria ndogo zinahitajika udhibiti maambukizo corona

**VITA** dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu (Covid-19) unaosababishwa na virusi vya corona, bado inaendelea nchini na duniani kwa ujumla.

Hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa kudhibiti maambukizo ya ugonjwa huo ambao hadi sasa umesababisha zaidi ya watu robo milioni kupoteza maisha na mamilioni kupata maambukizo.

Suala la kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya maambukizo ya ugonjwa huu ni muhimu muhimu kwa kila mmoja ili kulinda maisha yake na ya wengine.

Hivyo maelekezo na ushauri kutoka kwa wataalamu wa afya kuhusiana na tahadhari za kuchukua ni muhimu sana kufuatwa na kuzingatiwa bila kushurutishwa.

Kwa kukumbushia mambo muhimu ambayo wataalamu wa afya wanayahimiza kama tahadhari dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona ni kunawa mikono na sehemu zingine za mwili ambazo ni rahisi kusababisha maambukizo kwa kutumia maji tiririka na sabuni.

Aidha, kutumia vitakasa mikoni, uvaaji wa barakoa, kuepuka kushikana mikono na pamoja na kuepukana na mikusanyiko.

Hata hivyo, pamoja na elimu inayotolewa na wataalamu pamoja na msisitizo wa kuchukua tahadhari hizo, bado sehemu kubwa ya jamii haionekani kuchukua tahadhari.

Kwa mfano, watu wengi kwenye maeneo kadhaa hawavai barakoa na wanaendelea kukaa kwenye mikusanyoko katika maeneo ya masoko, vijiweni, kwenye minada na mitaani.

Hali hiyo inatishia usalama wao wenyewe na wa wengine ambao wanajitahidi kuchukua tahadhari zinazoshauriwa na kuhimizwa na wataalamu wa afya.

Ni jambo la kushukuru kwamba serikali yetu mbali na kutotangaza hali ya dharura ya kufungia watu ndani, lakini pia imejiweka kando na matumizi ya nguvu dhidi ya watu ambao hawafuati maelekezo ya tahadhari dhidi ya kusambaa kwa virusi vya corona.

Itakumbukwa jinsi ambavyo baadhi ya nchi duniani zilivyolazimika kutumia nguvu ya dola dhidi ya wakaidi wa 'lockdown' na marufuku nyingine. Hilo lilipaswa kutupa funzo la kuheshimu na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na serikali yetu.

Kama ukaidi huo utaendelea, serikali inaweza kuamua kutumia nguvu zake dhidi ya wakaidi, hivyo, tunatoa angalizo kwamba kila mmoja popote alipo ahakikishe kuwa anachukua tahadhari kwa mujibu wa maelekezo ya wataalamu wa afya na serikali dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona.

Tunazikumbusha halmashauri zetu za miji, wilaya, manispaa na majiji, mbali ya kutoa elimu ya kujikonga dhidi ya maambukizo hayo, zitumie sheria ndogo zilizopo na ikiwezekana kutunga mpya kwa ajili ya kudhibiti maambukizo ya janga hilo.

Sheria hizo pamoja na mambo mengine, zitasaidia kuwawezesha wananchi kwa elimu juu ya kujikinga na maambukizo na vile vile kuwaadabisha wanaokaidi maelekezo yanayotolewa na mamlaka za serikali na wataalamu wa afya.

Tumezisikia baadhi ya halmashauri nchini zilianza kuzitumisha sheria hizo wakati huu wa tishio la virusi vya corona. Kwa mfano, mwishoni mwa wiki hii, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani ilitangaza kuwakamata na kuwapa adhabu ya kufanya usafi wa mazingira vijana watakaokutwa kwenye mikusanyiko.

Mkuu wa Wilaya hiyo alisema kuwa vijana wengi wamekuwa wakikaa kwenye mikusanyiko katika maeneo ya vijiweni. Licha ya kupewa elimu ya kuepukana na mikusanyiko.

Kutokana na ukaidi huo, alisema wataanza kuwakamata na kuwapeleka kwenye maeneo ya masoko na ofisi za umma kwa ajili ya kufanya usafi na mwisho wa siku wanawaachia kurejea makwao.

Tunashauri kuwa halmashauri zote zingine zitumie sheria hizo ndogo kwa kuwa tunaamini zitasaidia katika kipindi hiki cha vita dhidi ya corona.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Kushughulikiana huku kutaleta kujidhoofisha

Na Sabato Kasika

**CHAMA** cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimewafukuza uanachama wabunge wanne, huku wengine 11 wakitakiwa kujieleza kwa nini wasichukuliwe hatua za kinidhamu.

Hiyo, inatokana na wabunge hao kuhudhuria vikao vya bunge badala ya kujiweka eneo la kujitenga kwa siku 14 kama ambavyo chama kiliagiza, lakini wao wakakiuka maelekezo hayo.

Wabunge waliofukuzwa katika chama hicho ni Antony Komu (Moshi Vijijini), Joseph Selasini (Rombo), wote kutoka mkoani Kilimanjaro, Wilfred Rwakatare (Bukoba Mjini), Kagera na David Silinde(Mbozi) mkoani Songwe.

Aidha, wanaotakiwa kujieleza ni wabunge wa Viti Maalum Suzan Masele, Joyce Sokombi, Rose Kamili, Latifa Chande, Lucy Mlowe, Sware Semesi, Sabrina Sungura na Anne Gideria.

Mbali na hao, pia mbunge wa Moshi Mjini, Jaffary Michael, wa Kilombero, Peter Lijualikali na Karatu, William Kambalo, hali ambayo inaonyesha mpasuko ndani ya chama hicho.

Chama hicho kimewafukuza uanachama wabunge wanne, huku wengine 11 wakitakiwa kujieleza kwa nini wasichukuliwe hatua za kinidhamu, kufuatia hatua yao ya kuhudhuria vikao vya bunge badala ya kujitenga.

Huenda hatua hiyo ya Chadema inaweza kusababisha sintofahamu hasa wakati huu ambao nchi inaelekea kwenye uchaguzi mkuu, na chama hicho nacho kinajiandaa kushiriki .

Ninasema hivyo, kwa sababu suala la msamaha na maelewano katika chama ni la muhimu kwa ajili ya kuimarisha kuliko kuchukua hatua za kufukuzana kipindi hiki ambacho umoja unahitajika zaidi.

Nchi inaelekea katika uchaguzi mkuu, hivyo hatua zozote zinatakiwa kuchukuliwa kwa umakini kwa lengo la kujenga chama kuliko kukifanya watu wakione siyo sehemu ya sahihi ya kuendesha siasa.

Vinginevyo Chadema inaweza kuingia kwenye uchaguzi mkuu ikiwa vipande vipande, hali ambayo si salama kwa uhai wa kisiasa wa chama hicho kikubwa cha upinzani nchini.

Waswahili wanasema kwamba, 'umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu', hivyo Chadema kufukuza wanachama wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu ni kujiongezea udhaifu.

Kipindi hiki kilikuwa ni nafasi nzuri kwa chama kujipanga na kujiimarisha zaidi badala ya kufukuzana, hali ambayo kwa namna moja au nyingine inaweza kusababisha kiyumbe, kwani chama ni wanachama.

Ndiyo, chama kina katiba, kanuni na miongozo yake, lakini uamuzi uliochukuliwa kipindi hiki cha kuelekea katika uchaguzi unaweza kukidhoofisha, kwani waweza kuwa faida kwa vyama vingine.

Umoja imara ndani ya chama ndiyo unaoweza kufanya vyama vikaungana kama ilivyotokea vikaanzisha Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) ambao ulichangia kuvifanya vipate wabunge na madiwani wengi mwaka 2015.

Kwa hiyo mtazamo wa vyama vya upinzani ungekuwa ni kutafuta jinsi ya kujiimarisha zaidi hata kama vinakutana na changamoto kama hizo ambazo zingeweza kuvumiliwa wakati huu wa kuelekea katika uchaguzi mkuu.

Siyo siri kwamba kwenye msafara wa mamba, kenge huwa pia wamo, hivyo hata katika chama, wasaliti pia huwa wamo, lakini zinahitajika mbinu zaidi za kuwashughulikia kwa lengo la kuimarisha umoja katika chama.

Ikumbukwe kwamba Januari mwaka huu, chama hicho kilifungua pazia kwa wanachama wake wanaotaka kuwania ubunge na udiwani kuandika barua za maombi katika maeneo yao ili wajadiliwe na vikao maalum.

Mchakato huo umefanyika kwa lengo la kuhakikisha chama hicho kinapata wanachama ambao kinaamini hawawezi kukiangusha kwenye uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, zaidi ya wanachama 70 walijitokeza kuomba kuwania na ubunge na udiwani katika maeneo mbalimbali nchini.

Hatua hiyo ya kujitokeza wanachama wengi kuomba kuwania nafasi za uongozi katika uchaguzi ujao, inaelezwa na Mrema kwamba chama hicho kinazidi kupendwa, na kwamba chama hicho kinafanya mambo kwa uwazi.

Kwamba kilitangaza mchakato huo wanachama wakajitokeza na sasa kimeshafunga rasmi pazi, na kilichobaki ni taratibu nyingine za kufanikisha mchakato huo, ili kupata wanachama sahihi wa kukiwakilisha.

Hivyo nguvu kubwa zingeelekezwa katika mchakato huo na kufikia mengine yanayojitokeza hadi kuhakikisha uchaguzi mkuu unapita kwanza, kwa kutambua kwamba kwenye msafara wa 'mamba, kenge hawakosekani'.

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA KILIMO



*Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga (Mb)*
*Waziri wa KILIMO*



*Mhe. Omary Tebweta Mgumba (Mb)*
*Naibu Waziri KILIMO*



*Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb)*
*Naibu Waziri KILIMO*



*Bwana. Gerald Musabila Kusaya–*
*Katibu Mkuu KILIMO*



*Prof. Siza Donald Tumbo –*
*Naibu Katibu Mkuu KILIMO*

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2020/2021**

# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2020/2021

## 1. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Kilimo (Fungu 43), Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (Fungu 05) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (Fungu 24) mnamo tarehe 25 na 26 Machi, 2020 Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuendelea kuijaalia nchi yetu amani, utulivu na mshikamano na kutuwezesha kushiriki katika mkutano huu wa Bunge la 19 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni mkutano wa mwisho katika uhai wa Bunge la 11.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kusimamia Kilimo ambacho ndio tegemeo la Watanzania walio wengi. Vilevile, niwashukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanayofanya kusukuma maendeleo ya nchi hii, ikiwemo Sekta ya Kilimo. Aidha, binafsi ninawashukuru viongozi wangu wote kwa maelekezo, ushauri na miongozo wanayonipatia ambayo imenisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine naomba kumpongeza Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 1 Aprili, 2020. Hotuba hiyo iligusa maeneo mengi ikiwemo Sekta ya Kilimo ambapo alisisitiza uimarishaji wa huduma za ugani, kilimo cha umwagiliaji, ushirika, upatikanaji wa pembejeo sahihi na miundombinu ya masoko.

Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Hussein Mohammed Bashe (Mb.) kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri na Ndugu Gerald M. Kusaya kuwa Katibu Mkuu katika Wizara ya Kilimo na kuungana na viongozi wengine wa wizara kusukuma kilimo hapa nchini.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, na Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.) pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyolisimamia na kuliendesha Bunge letu tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Aidha, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa kazi nzuri walizozifanya katika miaka hii mitano ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili. Nimpongeze pia Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu Mbunge wa Singida Mashariki kwa kuchaguliwa kujiunga na Bunge lako Tukufu.

6. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene Mbunge wa jimbo la Kibakwe kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu Mbunge wa jimbo la Ilala kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Mbunge wa Iramba Magharibi kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Bunge lako Tukufu limewapoteza Wawakilishi wenzetu wanne ambao ni Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Newala Vijijini aliyefariki tarehe 15 Januari 2020, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare Mbunge wa Viti Maalum aliyefariki tarehe 20 Aprili, 2020, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa Mbunge wa Sumve aliyefariki tarehe 29 Aprili, 2020 na Mheshimiwa Balozi Dkt Augustine Philip Mahiga (Mb) aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria aliyefariki tarehe 1 Mei, 2020. Nitumie fursa hii kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, Chama cha Mapinduzi, familia za marehemu, ndugu, jamaa na wananchi wa majimbo ya Newala Vijijini na Sumve.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa jimbo la Mufindi Kaskazini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma Mbunge wa Viti Maalum kwa ushirikiano na ushauri mzuri walioutoa katika kipindi chote cha mwaka 2019/2020 pamoja na kuipitia taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2019/2020 na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2020/2021. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, ushauri wao umezingatiwa na tutaendelea kushirikiana na Kamati ili kuleta mageuzi ya kilimo na kufikia matarajio ya wananchi katika kufikia uchumi wa kati.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani zangu za pekee kwa Wananchi wa Jimbo la Vwawa kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Napenda kuwahimiza kuendelea kuniamini na kuiamini Serikali ya Awamu ya Tano na kwamba maendeleo ya Jimbo letu yanategemea sana kufanya kazi kwa pamoja. Aidha kwa namna ya pekee ninawapongeza sana Naibu mawaziri Mh. Omary Tebweta Mgumba (Mb) na Hussein Mohamed Bashe (Mb) kwa jinsi wanavyonisaidia katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Wizara ya Kilimo. Vile nawapongeza Katibu mkuu Ndugu Gerald Kusaya, Naibu katibu Mkuu. Prof. Siza Tumbo, wakurugenzi na vitengo, wakuu wa Taasisi, Bodi na wakala zilizo chini ya wizara kwa ushirikiano na kazi nzuri wanazoendeleza kuzitekeleza ili kufanikisha malengo ya kilimo nchini.

10. ***Mheshimiwa Spika***, Awali ya yote nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa msukumo wa kuendeleza Sekta ya Kilimo. Aidha, katika hotuba yake aliyoitoa tarehe 20 Novemba, 2015 akifungua rasmi Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Dodoma alisisitiza kutekeleza ahadi alizozitoa kwa wakulima kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015-2020. Wizara imetekeleza ahadi hizo kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) na kuwezesha kilimo kuchangia katika uchumi na maendeleo ya Taifa letu, hususan katika maeneo ya usalama wa chakula na lishe, ajira, upatikanaji wa malighafi za viwanda na kuchangia katika kupunguza umaskini na kuongeza kipato cha wakulima.

11. ***Mheshimiwa Spika***, baadhi ya ahadi alizotoa ni pamoja na kuimarisha huduma za ugani, upatikanaji na usambazaji wa pembejeo, zana za kisasa za kilimo, masoko ya uhakika ya mazao, kuimarisha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kilimo na kuondoa ushuru, kodi na tozo ambazo ni kero kwa ajili ya maendeleo ya kilimo.

## 2. MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA UCHUMI

12. ***Mheshimiwa Spika***, kilimo kimeendelea kuwa ni mhimili muhimu katika maendeleo ya uchumi wa taifa letu. Katika kipindi cha miaka mitano, Pato la Taifa linalotokana na kilimo, kwa kutumia bei za Mwaka 2015 limeongezeka kwa asilimia 17 kutoka shilingi trilioni 25.2 Mwaka 2015 hadi shilingi trilioni 29.5 Mwaka 2019. Vilevile, sekta imeendelea kutoa ajira kwa Watanzania kwa asilimia 58 Mwaka 2018, imechangia asilimia 28.2 ya Pato la Taifa ambapo sekta ndogo ya mazao imechangia asilimia 16.2. Hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwemo vyakula vinavyotokana na mazao ya kilimo. Aidha, kati ya mwaka 2015 hadi 2019 sekta ya kilimo imeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.2 ambapo sekta ndogo ya mazao imeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.8.

## 3. MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2019/2020

### *3.1 Fedha Zilizoidhinishwa*

13. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Kilimo kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya Shilingi **bilioni 253.86** ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi **bilioni 77.78** ni kwa matumizi ya kawaida na Shilingi **bilioni 176.08** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

## 4. HOMA KALI YA MAPAFU (COVID-19)

14. ***Mheshimiwa Spika,*** mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID-19) unaosababishwa na virusi vya Corona umeathiri sekta mbalimbali za kiuchumi nchini ikiwemo sekta ndogo ya mazao. Tathmini

# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO

imefanyika na kubaini kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2019/2020 haujaathirika kwa kuwa pembejeo zimeshawasili nchini.

Aidha, katika kukabiliana na uhaba wa mbolea unaoweza kutokea kutokana na kuendelea kuwepo kwa tatizo la COVID-19, Wizara imeiagiza TFRA kuhakikisha mbolea zote zinaagizwa mapema kipindi hiki kabla ya msimu ujao kuanza.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** mazao ya asili ya biashara ambayo ni pamba, korosho na kahawa misimu yake ya mauzo imeishia mwezi Machi, 2020 na hivyo kutoathirika na ugonjwa huo. Aidha, kwa zao la tumbaku wakulima wameshafunga mikataba na wanunuzi kwa ajili ya msimu 2020/21 na hivyo kutoathiriwa na Covid-19. Mazao ambayo yameonesha dalili za kuathirika ni chai na mazao ya bustani ambayo masoko na usafirishaji wake nje ya nchi umeathiriwa. Vilevile, ugonjwa wa COVID-19 iwapo utaendelea kwa muda mrefu unaweza ukaathiri soko la pamba, korosho, kahawa, na mazao mengine yanategemea minada ya moja kwa moja.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na ugonjwa wa COVID-19, serikali imepanga kununua tani 300,000 za chakula kupitia NFRA, kuhakikisha sekta binafsi zinahifadhi kwenye maghala, kutumia mfumo wa Soko la Bidhaa (TMX) kwa mazao ambayo hutegemea zaidi wanunuzi kutoka nje ya nchi kama vile zao la korosho, kahawa, pamba, n.k., kutumia balozi zetu nje ya nchi kutafuta manunuzi na masoko, na kutumia soko la moja kwa moja, n.k. hivyo kwenye upande wa mazao ya chakula hii ni fursa ya kuweza kuuza Zaidi kuliko muda mwingine.

*Utekelezaji wa Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2019/2020*

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kutekeleza maeneo ya kipaumbele ya kuongeza uzalishaji na tija kwenye kilimo kwa kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, udhibiti wa visumbufu, matumizi ya zana bora za kilimo na huduma za ugani; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo na masoko; kufanya utafiti wa kilimo na kuzalisha teknolojia kwa mazao ya mahindi, muhogo, ngano, michikichi, ufuta, alizeti, pamba na mpunga.

## 5. MAFANIKIO YA WIZARA YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA SERIKALI YA AWAMU YA TANO

**18.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha miaka minne Wizara imepata mafanikio makubwa katika maeneo ya usalama wa chakula na lishe; uzalishaji wa mazao makuu ya biashara; upatikanaji wa pembejeo za kilimo; viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na masoko; utafiti, huduma za ugani na mafunzo; hifadhi ya mazao; uzalishaji wa mazao ya bustani; kuimarika kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko; kuimarika kwa ushirika; kuimarika kwa kilimo cha umwagiliaji; ongezeko la ushiriki wa vijana katika kilimo; matumizi bora ya ardhi; kuhuisha mifumo na sera za kilimo na kuanzishwa kwa kanzidata ya wakulima na wadau mbalimbali wa kilimo.

### 5.1 Usalama wa Chakula na Lishe

**19.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha miaka minne (4) upatikanaji wa chakula umeendelea kuimarika na hivyo kuwezesha nchi yetu kujitosheleza kwa chakula kwa wastani wa asilimia 121 na kuwa na wastani wa ziada ya tani 2,798,700.60. Aidha katika mwaka 2019/2020 upatikanaji wa chakula ulifikia tani milioni 16.2 ukilinganisha na mahitaji ya chakula ya tani milioni 13.8. Hivyo ziada ya chakula ilikuwa tani 2,473,774 na kuwa na kiwango cha utoshelevu cha asilimia 118.

*Hali ya Lishe nchini*

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** kulingana na taarifa ya mapitio ya kati (Mid Term Review) ya hali ya lishe nchini katika utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa lishe wa mwaka 2016-2021) uliyofanyika mwaka 2019, inaonesha kuwa udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano umepungua kutoka asilimia 34 mwaka 2015 kufikia asilimia 32 mwaka 2018. Aidha, Kiwango cha ukondefu kwa watoto chini ya miaka mitano kitaifa kimeendelea kushuka kutoka asilimia 3.8 hadi asilimia 3.5 na pia upungufu wa damu kwa akina mama umepungua kutoka asilimi 44.7 hadi kufikia asilimia 28.7 kwa kipindi hicho.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu la serikali ni kuhakikisha kuwa mazao mbalimbali ya chakula yenye virutubishi kwa wingi yanazalishwa yakiwemo viazi lishe" na maharagwe yaliyoongezewa madini chuma na zinki. Uzalishaji na utumiaji wa mazao haya unachangia kupunguza tatizo la upungufu wa damu unaosababishwa na ukosefu wa madini chuma na tatizo la upungufu wa vitamin A hususan kwa akina mama walio katika umri wa kuzaa na watoto chini ya miaka mitano ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 12 hadi 15 wa kitabu cha Hotuba).***

### 5.2 Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao makuu ya biashara yakiwemo pamba, kahawa, chai, pareto, tumbaku, korosho, mkonge na miwa umeongezeka kutoka jumla ya tani 796,502 Mwaka 2015/2016 hadi jumla ya tani 1,144,631 Mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 43.7. Aidha zao la miwa limeongoza likifuatiwa na korosho na Pamba.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile katika kipindi hicho cha miaka minne kiasi cha tani 1,613,000 za mazao ya kahawa, pamba, katani, chai, tumbaku na korosho kiliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa jumla ya Dola za Marekani Milioni 3,419.77 sawa na Shilingi trilioni 6.9. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku imeuza jumla ya tani 500 za tumbaku ya daraja la chini (Reject) ambayo mapato yake yamesaidia kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima na kuwaongezea kipato. ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 15 hadi 16 wa kitabu cha Hotuba)***

### 5.3 Uzalishaji wa Miwa na Sukari

**24.** ***Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika,*** Mahitaji ya sukari nchini ni takribani tani 420,000 ikiwa ni wastani wa tani 35,000 kwa mwezi. Uzalishaji wa Sukari kwa mwaka 2019/2020 ulikadiliwa kuwa tani 380,000, kulingana na matarajio ya uzalishaji huo upungufu wa Sukari ulikadiliwa kuwa wastani wa tani 40,000 kwa matarajio kwamba viwanda vingeweza kuzalisha kiasi chote cha Sukari cha tani 380,000 kilichokadiliwa mwanzoni mwa msimu. Aidha, kutokana na mvua kunyesha kupita kiasi viwanda havikufikia Malengo ya uzalishaji ambapo vilizalisha tani 310,000 hivyo pengo la mahitaji kuongezeka kutoka tani 40,000 hadi kufikia tani 110,000. Hata hivyo, kwa vile viwanda vya ndani vinatarajia kuanza uzalisha mwezi Juni, 2020 ni matarajio ya serikali upatikanaji wa Sukari utarejea katika hali yake ya kawaida.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kukabiliana na upungufu huo, Serikali ilichukua hatua ya kutoa vibali vya tani 40,000 kwa wazalishaji wa ndani wanne (4) kuingiza Sukari ambapo kila mzalishaji alipewa kibali cha kuingiza tani 10,000. Hadi sasa kiasi cha tani 14,398 kimekwisha ingizwa na kusambazwa nchini, kiasi cha tani 3,920 kipo katika hatua mbalimbali za kutolewa bandarini na kiasi cha tani 21,166 kinatarajiwa kuingizwa nchini kabla ya mwisho wa mwezi Mei, 2020. Kutokana na tatizo la mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 wafanyabiashara wachache wasio waadilifu wamekuwa wakihodhi Sukari na kusababisha kupanda bei. Hata hivyo, serikali inafuatilia mwenendo wa uingizwaji wa Sukari na kuchukua hatua madhubuti ili kuhakikisha kunakuwa na utulivu wa soko.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inalenga kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 320,000 za sasa hadi 630,000 ifikapo mwaka 2024/2025 kutokana na uwekezaji mpya na upanuzi wa viwanda vilivyopo na hivyo kujitosheleza kwa mahitaji ya Sukari nchini. Hata hivyo, serikali itaendelea kutoa vibali vya kuziba pengo la uzalishaji Sukari nchini kwa wakati ilikuhakikisha Sukari inapatikana nchini kwa wakati wote.

### 5.4 Mazao ya Bustani

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka tani 5,931,900 mwaka 2015/2016 hadi tani 6,556,102 mwaka 2018/2019. Thamani ya mauzo ya mazao ya bustani yakiwemo mbogamboga na maua nje ya nchi yameongezeka toka Dola za Marekani milioni 412 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani milioni 779 mwaka 2018/2019. Ongezeko hilo la mauzo linaifanya Tasnia ya mazao ya bustani kuchangia asilimia 38 ya fedha za kigeni zinazotokana na sekta ya kilimo.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi hicho, uwekezaji katika mazao ya bustani kupitia sekta binafsi chini ya mwamvuli wa TAHA umefikia Dola za Marekani milioni 30. Aidha zao la parachichi limeonesha mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka minne ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 20,000 Mwaka 2015 hadi kufikia tani 190,000 Mwaka 2018. Mauzo yenye thamani ya Dola za marekani Milioni 8.5 yamefanyika katika soko la ulaya hususan nchi za Ufaransa, Uholanzi na Uingereza. ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 17 hadi 20 wa kitabu cha Hotuba)***

### 5.5 Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO

*5.5.1 Mbegu*

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne upatikanaji wa mbegu bora umeongezeka kutoka tani 36,614.28 mwaka 2015/2016 hadi tani 76,725.52 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 110. Aidha, uzalishaji wa ndani wa mbegu bora umeongezeka kutoka tani 20,604.97 mwaka 2015/2016 hadi tani 69,173.17 mwaka 2019/2020. Vilevile, uzalishaji wa miche umeongezeka kutoka miche 5,000,000 mwaka 2015/16 hadi kufikia miche 25,285,859 mwaka 2019/20. Pamoja na mambo mengine, mafanikio hayo yametokana na kuongezeka kwa eneo la uzalishaji wa mbegu na miche kutoka hekta 10,887 hadi hekta 94,368. Vile vile serikali imeimarisha maabara ya TOSCI na hivyo kupata ithibati ya Shirika la Kimataifa la Uthibiti wa Ubora wa Mbegu (International Seeds Testing Association – ISTA) pamoja na kujiunga na Skimu za Mbegu za Shirika la Kimataifa (OECD Seed Schemes) ambayo itaiwezesha nchi kufanya biashara ya mbegu kimataifa.

*5.5.2 Mbolea*

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho Wizara imeimarisha upatikanaji wa mbolea nchini kwa kuanzisha mfumo wa ununuzi wa pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*) ambao umewezesha kuongeza upatikanaji wa mbolea kutoka tani 302,482 mwaka 2015/2016 hadi 633,197 mwaka 2019/2020. Mfumo huo umewezesha wakulima kupata mbolea kwa wakati na bei nafuu. Aidha, idadi ya viwanda vinavyotengeneza mbolea na visaidizi vya mbolea (*fertilizer suppliment*) vimeongezeka kutoka viwanda vinne (4) mwaka 2015 hadi viwanda 13 mwaka 2019. Kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili (2) ni vya visaidizi na 11 ni vya mbolea.

*5.5.3 Viuatilifu*

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Upatikanaji wa viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya milipuko kama vile panya, nzige, kweleakwelea na viwavijeshi vamizi umeongezeka kutoka tani 4,111.50 mwaka 2015 hadi tani 16,869.10 mwaka 2019. ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 21 hadi 26 wa kitabu cha Hotuba)***

**5.6 Mazingira ya Uwekezaji na Uanzishaji wa Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Kilimo**

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2015/16 hadi 2019/20, Serikali imefuta ushuru, tozo na ada 105 na kupunguza tozo nne (4) kati ya 146 zilizokuwa zinatozwa katika mazao ya kilimo. Hatua hiyo imevutia Sekta binafsi kuwekeza takribani Shilingi Trilioni 3.7 kwenye mnyororo wa thamani wa kuendeleza mazao ya chai, kahawa, mkonge, ngano, shayiri na mpunga. Aidha, ajira katika mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo zimeongezeka kutoka wastani wa ajira 3,880,262 Mwaka 2015/16 hadi kufikia wastani wa ajira 5,204,607 Mwaka 2018/19.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imehamasisha ujenzi wa viwanda ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na kutengeneza ajira kwa watanzania. Katika kipindi cha miaka minne, jumla ya viwanda vipya 189 vya kuchakata mazao vimeanzishwa vikiwemo vya korosho 9, chai 3, kahawa 59, pamba 36, mkonge 81 na pareto 1. ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 29 hadi 31 wa kitabu cha Hotuba)***

**5.7 Upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne (4) Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi. Katika kufikia azma hiyo, Wizara imeanzisha kitengo cha Masoko (Agricultural Marketing Division) katika Idara ya Maendeleo ya Mazao inayosimamia utafutaji wa masoko, kufanya tafiti za masoko na bei za mazao pamoja na kufuatilia mifumo ya uuzaji wa mazao. ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 33 hadi 36 wa kitabu cha Hotuba)***

**5.8 Utafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya Kilimo**

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi hicho TARI kwa kushirikiana na sekta binafsi imegundua aina 124 za mbegu bora**.** Aidha, kati ya hizo kampuni binafsi zimegundua aina 35 za mbegu bora za mazao ya kilimo. Vilevile, utafiti wa kupima afya ya udongo na kuandaa ramani zinazoonesha mtawanyiko na viwango vya mboji (Organic carbon) pamoja na uchachu (pH) wa udongo katika mikoa yote nchini umefanyika.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia vyuo vyake 14 imetoa wataalam wa kilimo 7,530 na 6,146 wamehitimu katika vyuo binafsi 12 ngazi ya Astashahada na Stashahada za kilimo. Aidha, jumla ya maafisa ugani 902 na wakulima 42,192 wamepatiwa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora, teknolojia mbalimbali za uzalishaji, jinsia na masoko. ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 37 hadi 40 wa kitabu cha Hotuba)***

**5.9 Hifadhi ya mazao**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2015 nchi ilikuwa na jumla ya maghala 3,400 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,774,106 za mazao ya chakula. ujenzi na kukarabati miundombinu ya hifadhi yavihenge 57 na ghala 118 zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 203,000 na tani 100,700 mtawalia na hivyo kuongeza uwezo wa kuhifadhi kutoka tani 2,774,106 mwaka 2015/2016 hadi tani 3,077,806 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 11. ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 40 hadi 46 wa kitabu cha Hotuba)***

**5.10 Kuimarisha Ushirika**

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ushirika umeendelea kuimarika ambapo Vyama vya Ushirika vimeongezeka kutoka 7,394 mwaka 2015 hadi 11,626 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 57. Vilevile, idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka 2,390,593 mwaka 2015 hadi 5,880,736 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 146. Hata hivyo, Wizara imechukua hatua ya kuvifuta jumla ya Vyama 3,348 ambavyo vilibainika kuwa ni hewa na hivyo kubaki na jumla ya Vyama vya ushirika 8,611 kwenye daftari/rejista ya Vyama vya ushirika nchini.

***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 46 hadi 48 wa kitabu cha Hotuba)***

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, thamani ya mikopo inayotolewa na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 899.2 mwaka 2015 hadi Shilingi trilioni 1.5 mwezi Machi, 2020. Aidha, idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka viwanda 304 mwaka 2015 hadi viwanda 379 mwaka 2019.

**5.11 Kilimo cha Umwagiliaji**

**40.** ***Mheshimiwa Spika*****,** eneo la kilimo cha umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 461,326 mwaka 2015/2016 hadi hekta 694,715 mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 33.6. Aidha, tija ya uzalishaji katika skimu za umwagiliaji zilizoendelezwa imeongezeka kutoka wastani wa tani 1.8 – 2.0 kwa hekta mwaka 2015/2016 hadi kufikia wastani wa tani 4.0 – 5.0 kwa hekta 2019/2020 kwa zao la mpunga.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha miradi 179 iliyogharimu shilingi 96,188,597,689.55 imetekelezwa. Kati ya miradi hiyo, miradi 56 inasubiri kuzinduliwa. Miradi iliyokamilika ni pamoja na mradi wa uboreshaji miundombinu ya skimu ya umwagiliaji ya Dakawa yenye ukubwa wa hekta 2,000 iliyogharimu Shilingi 21,156,050,278; Skimu 9 kati ya skimu 16 zenye ukubwa wa hekta 2,547 za Mradi wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo (SSIDP); ukarabati wa miradi 4 ya skimu za umwagiliaji zenye jumla ya ukubwa wa hekta 2,000 iliyogharimu shilingi 1,166,220,000. ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 48 hadi 50 wa kitabu cha Hotuba)***

**5.12 Mfumo wa Vibali kwa Njia ya Kielektroniki (ATMIS)**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** mfumo wa vibali kwa njia ya kielektroniki (ATMIS) unaolenga kutoa huduma za utoaji vyeti vya usafi wa mazao ya mimea na vibali vya kuingiza na kuuza mazao nje ya nchi umeanzishwa. Mfumo huo umepunguza muda wa kupata kibali kutoka siku saba (7) za awali hadi siku moja (1) kwa wafanyabiashara. Vilevile, umechangia kudhibiti mianya ya udanganyifu wa nyaraka na kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

**5.13 Uanzishwaji wa Kanzidata ya Wakulima**

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa Usajili wa Wakulima (*Farmers Registration System-FRS*) na kutengeneza kanzidata ya wakulima ambayo itasaidia kuwatambua na kuwapatia vitambulisho, kuainisha mahitaji yao ikiwemo pembejeo za kilimo, huduma za kifedha na masoko na hatimae kuweka mipango ya kuwahudumia umeanzishwa. Hadi Aprili, 2020 jumla ya wakulima 1,275,220 (88.1%) katika mazao

# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO

nane makuu ya kibiashara ambayo ni korosho, pamba, kahawa, chai, mkonge, pareto, tumbaku na sukari wamesajiliwa kupitia mfumo huo.

**5.14 Bima ya mazao**

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** serikali kwa kushirikiana na wadau wa huduma za Bima ikiwemo Mamlaka ya Kudhibiti Shughuli za Bima nchini (TIRA), Shirika la Bima la Taifa (NIC), kampuni binafsi tano (5) za bima zimeanzisha Bima ya Mazao kwa lengo la kumsadia mkulima kujikinga na athari za majanga ya asili na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kupata dhamana ya mkopo.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha mfumo wa kuwasajili wadau wote wa sekta ya kilimo ikiwemo Sekta Binafsi *(Stakeholders mapping)*. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, jumla ya wadau wa sekta binafsi 564 wamesajiliwa ambapo Wazalishaji na wasambazaji wa pembejeo ni 198, Wazalishaji wa bidhaa za kilimo 103 na wasindikaji 363. Aidha, jumla ya miradi 105 inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo yenye thamani ya Shilingi Trilioni 3.3 imesajiliwa kwenye mfumo. Mfumo huo utaiwezesha Serikali kutambua juhudi na uwekezaji wa wadau wote na kuimarisha ushirikiano kati yao na Serikali katika kuendeleza sekta ya kilimo. ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 55 hadi 58 wa kitabu cha Hotuba)***

**6. MALENGO KWA MWAKA 2020/2021**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kutekeleza Maeneo 10 ya vipaumbele kupitia Fungu 43, 24 na 05 katika Idara, Vitengo, Tume na Taasisi za Wizara. Mpango wa bajeti umeweka msisitizo kwenye kilimo kitakachohakikisha upatikanji wa chakula cha kutosha, upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda na kufanya kilimo cha kibiashara.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maeneo ya kipaumbele ni pamoja na Kuendelea na utekelezaji wa Progamu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II); Kuboresha mifumo ya kitaasisi, Bodi na Sheria za Kilimo, kupata ujuzi na maarifa ya kilimo chenye tija, kurahisisha upatikanaji wa huduma za pembejeo na masoko; Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, maghala, masoko na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo; na Kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za mazao na upatikanaji wa pembejeo nyingine za kilimo na kuzisambaza kwa wakulima.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara imepanga kutekeleza malengo na shabaha zifuatazo; kuzalisha tani 18,000,000 za mazao ya chakula; kuzalisha jumla ya **tani 5,269,858** za mazao ya asili ya biashara yakiwemo pamba (400,000), korosho (300,000), chai (40,000), kahawa (90,000), miwa (4,246,630), pareto (2,800), mkonge (125,428) na tumbaku (65,000); Kuhakikisha upatikanaji wa mbolea tani 760,000; Kuhakikisha upatikanaji wa Mbegu tani 115,000; Kuhakikisha upatikanaji wa Viuatilifu tani 22,000; Kuzalisha tani 8,500,000 za mazao ya bustani; Kuhifadhi chakula kiasi cha tani 300,000; Kusimamia utafutaji na upatikanaji wa masoko ya mazao ya wakulima; Kununua na kuuza tani 500,000 za nafaka na tani 1,200,000 za muhogo mkavu kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB). Aidha, wanafunzi 2,600 kupitia vyuo 14 vya mafunzo ya kilimo watadahiliwa (MATIs); Kukarabati vyuo tisa (9) vya mafunzo ya Kilimo na Vituo vya utafiti wa kilimo vinne (5) na Kuendelea na zoezi la usajili wa Wakulima katika mazao mengine pamoja na usajili wa wadau wa kilimo.

**49.** ***Mheshimiwa Spika*** pia wizara itakamilisha ujenzi na ukarabati wa skimu 17 za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 8,536; kukamilisha usanifu na upembuzi wa skimu ya Mkombozi-Iringa (hekta 10,000), mabwawa na skimu za Luiche-Kigoma (hekta 3,000) na Ibanda-Sengerema/Geita (hekta 1,200), skimu za Ilemba (Sumbawanga – hekta 800) na Makwale (Kyela – hekta 3,500) pamoja na mabwawa ya Nyisanzi (Chato – hekta 260), Kisese (Kondoa-hekta 2,000), Msia (Mbozi – hekta 100), Idudumo (Nzega-hekta 200) na Masasi (Chato – hekta 530);

na Kujenga maghala 12 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,000 na kufundisha vijana 400 kuhusu teknolojia ya vihenge vya kisasa kupitia mradi wa TANIPAC. ***(Mheshimiwa Spika maelezo ya kina yametolewa Uk. 89 hadi 123 wa kitabu cha Hotuba)***

**7. SHUKRANI**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijamaliza hotuba yangu naomba nitoe shukrani za dhati kwa taasisi, makundi, na wadau mbalimbali tunaoshirikiana katika kuendeleza kilimo cha Tanzania. Kwanza, ninawashukuru kwa dhati watumishi wote wa Wizara; na wadau wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2019/2020 pamoja na kuandaa Hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, nitaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2020/2021.

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia katika juhudi za kuendeleza kilimo. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Vietnam, Canada na Poland. Ninayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, ENABEL, GIZ, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, ILRI na CABI. Nyingine ni EAC, SADC, AVRDC, AGRA, KILIMO TRUST, CIP, CIAT/PABRA, UNEP, WARDA, Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA) na HELVETAS. Wadau wengine ni Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu (IRLCO-CSA),*Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust*, *Rockfeller Foundation, Clinton Foundation, Aga Khan Foundation, Unilever*, Kampuni za *TAHA fresh Limited, Africado na Rugwe Avocado Company*na Asasi zisizo za kiserikali nyingi ambazo hatuwezi kuzitaja zote hapa.

**52.** *Mheshimiwa Spika,*natoa shukrani za wakulima wote nchi nzima kwa kazi kubwa wanazofanya kuendeleza kilimo nchini. Ni wazi kuwa mafanikio haya makubwa ya kilimo yanatokana na jududi na ushirikiano mkubwa na serikali. Kipeke nirudie kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Vwawa kwa namna wanavyoniunga mkono na kunipa ushirikiano. Naomba wote watumbue kuwa kilimo ni chakula, maisha, uchumi, biashara, viwanda na ajira. 8. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

**8. MAOMBI YA FEDHA ZA BAJETI KWA MWAKA 2020/2021**

**8.1 Makusanyo ya Maduhuli**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi **5,793,400,000** kutokana na ada za ukaguzi wa mazao yanayouzwa nje ya nchi au kuingizwa nchini, uuzaji wa nyaraka za zabuni, ukodishaji wa mitambo ya Tume ya Umwagiliaji.

**8.2 Fedha kwa Mafungu yote (43, 24 na 05)**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **229,839,808,000** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 kama ifuatavyo;

***8.2.1 Fedha kwa Fungu 43***

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **202,504,117,000** kupitiaFungu 43 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **137,273,144,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo. Aidha, Shilingi **65,230,973,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi **43,599,187,000** ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi **21,631,786,450** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

***WWW8.2.2 Fedha kwa Fungu 05***

**56.** ***MheshimiwaNaibu Spika,*** jumla ya Shilingi **17,726,845,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **12,801,180,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na, Shilingi **4,925,665,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi **4,040,481,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Tume na Shilingi **885,184,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo.

***8.2.3 Fedha kwa Fungu 24***

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **9,608,846,000** zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **7,059,837,000**ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi **2,549,009,000**ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**58.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara: www.kilimo.go.tz

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** **NAOMBA KUTOA HOJA**

## Yanayowadhalilisha wanawake kwenye uchaguzi yakomeshwe



Ukurasa 14



Ukurasa 13


## Uchaguzi mkuu 2020 kinamama kubanwa na mifumo kandamizi?



BALOZI MAHIGA

# Mbobezi wa UDSM aliyetumika UN kuleta amani maeneo korofi

**Na Ani Jozeni**



Balozi Mahiga na Katibu Mkuu wa zamani wa UN, Ban Kin Moon. **PICHA: MTANDAO**

IKIWA ni mwendelezo wa makala zinazochambua wasifu wa Balozi Dk. Augustine Mahiga, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, zilizoanza Jumatano iliyopita, kwa kuangalia alikopitia kikazi. Bado zipo sifa lukuki, ikiwamo kuzama katika nadharia za uhusiano wa kimataifa, alizowahi kufundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam UDSM. Endelea...

LICHA ya undani wa maelezo kuhusu maisha ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Balozi Dk. Augustine Mahiga, bado kuna nafasi ya kutafakari maisha yake na nini aliwakilisha katika diplomasia na maeneo mengine ya maendeleo.

Hakuna wanadiplomasia wawili wanaofanana, au wakuu wa idara za Umoja wa Mataifa kutoka Tanzania wanaoweza kufanana. Kila mmoja anakuja na mchango wake na mwelekeo wake, unaofafanua alichokifanya na alama anazoziacha.

Kazi ya Dk. Mahiga katika miaka takriban 42 tangu aondoke Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1978 akiwa mhadhiri wa Taaluma ya Siasa na Utawala, ni ya aina yake.

Ni mmoja kati ya wasomi wa Chuo Kikuu UDSM walioondoka katika umri mdogo na kuingia anga tofauti za utumishi wa kimataifa.

Kwa sehemu kubwa ya uteuzi wa aina hiyo kwa upande wa wahadhiri chuoni hapo, mara nyingi zaidi mtaalamu husika anakuwa nje kwa muda halafu anaendelea na kazi chuoni.

Kuna kundi lingine la wasomi ambao wanateuliwa katika kazi za kitaifa na wasirudi tena chuoni, lakini mandhari yao ya kikazi kimsingi yanakuwa hapa nchini, kwa mfano kwa uteuzi wa kusimamia mashirika ya umma au wizara iwe ni ukatibu mkuu au uwaziri.

Wapo waliotoka katika ngazi kama hiyo na kurudi chuoni kwa muda mfupi halafu kuendelea na kazi za kitaifa, akiwamo Profesa Mark Mwandosya, mhandisi umeme aliyepata sifa lukuki katika masomo yake.

Akiwa amefikia ngazi ya ukatibu mkuu alirudi chuoni kufundisha, baadaye akawa mbunge na kuendelea na uwaziri na ukawa ndiyo mwisho kuwepo chuoni hapo.

Dk. Mahiga alikabidhiwa kazi zinazoendana na taaluma yake ya udadisi na uchambuzi wa kisiasa, aliyoianza akiwa mshauri Ikulu kabla ya kukabidhiwa makabrasha tofauti katika taasisi nyeti na punde akaonekana anaweza kujenga hoja na kuwezesha inachoamini Tanzania kielekweke, hivyo akawa ndiye mtu anayefaa kuchukua nafasi ya Dk. Salim Ahmed Salim kama balozi Umoja wa Mataifa.

Ni viatu ambavyo ingekuwa vigumu kwa mtu yeyote kuvivaa, na haikuwa jambo la kushangaza kuwa hapakuwa na 'bashasha' kama za Dk. Salim wakati wake, kwani mwanadiplomasia huyo alikonga nyoyo za dunia kwa suala la China.

Dk. Mahiga alikuwa katika kile Waingereza wanaita 'eye of the storm,' jicho la tufani, kwa muda wake wote wa utumishi serikalini na kama mtumishi wa kimataifa, kwa uteuzi wa makatibu wakuu tofauti wa Umoja wa Mataifa.

Kwa kuwa hakuwahi kusahaulika katika ngazi yoyote aliyofikia, akapewa jukumu moja baada ya jingine, yaani kutoka chuoni kuingia Ikulu, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, kuchukua nafasi ya Dk. Salim, halafu UN kumchukua na kubaki naye muongo mzima, si kazi rahisi.

Ni mtu aliyeaminika katika maeneo nyeti, na ni wazi alileta tija kuongea na watu wasioelewa diplomasia, katika vituo vigumu vya kazi kama Liberia na Somalia.

Kusema kweli, kazi hizo za upatanishi wakati wa vita zinahitaji mtu mtulivu ambaye yuko tayari kuhatarisha hata maisha yake ili kuokoa wengine endapo kwa juhudi zake urefu wa vita unaweza kupungua, au mifumo ya amani ikaharakishwa.

Kwa maana hiyo, hayati Dk. Mahiga ameitendea haki taaluma ya uelewa wa mifumo ya kiusalama katika maisha ya nchi na mazingira tofauti ya kimataifa, kuliko mwanadiplomasia mwingine ambaye nchi hii imewahi kuwa naye.

Hakuwa mtu aliyepewa tu kazi ya ubalozi ila alianza katika ushauri, na baada ya miaka 10 akiiwakilisha nchi, akawa sasa mshauri wa kimataifa. Alikuwa anabadilishiwa vituo vya kazi na siyo kupanda ngazi au kupata sifa.

Kwa maana hiyo haitakuwa sahihi kumlinganisha Dk. Mahiga na baadhi ya wale waliopewa nafasi kubwa UN kwani zaidi walikwenda kama watawala.

Hawakuingizwa katika maeneo ya misukosuko na vita yanayohitaji mtaalamu wa amani, kujenga hoja kwa taabu mbele ya watu wanaongoja kikao hicho kiishe waendelee na mipango yao ya mashambulizi.

Balozi Mahiga siyo tu alifanya kazi hiyo na 'Simba wa Liberia' halafu miongoni mwa wapiganaji 'vita isiyoisha' nchini Somalia na akawa anapata usinginzi anajiandaa kuketi mezani na watu hao hao kwa miaka kadhaa na UN ikawa tegemezi kwake hadi amefikia umri unaokaribia miaka 70 haikuwa mazingira ya kawaida.

Kimsingi ni kuwa Mahiga amethibitisha kuwa 'taaluma ya siasa' au ya amani' ni kitu gani, ila kuna ziada ambayo inabidi iandane na busara na hata imani.

Ni hali ambayo alikuwa anapewa kazi ambazo si wengi walikuwa wanazitaka na kwa hakika siyo wengi walikuwa wanaziweza, wadumu hapo na hata kufurahia kutoa mchango angalau kidogo kufikia amani. Hawakuwa wengi.



Kikosi cha walinzi wa GC wakiimarisha ulinzi kwenye gari ya Rais Kim Jong –un wa Korea Kaskazini. **PICHA: MTANDAO**

# Ndiyo uwezo, maajabu ya walinzi wa Kim Jong-un

**Na Joseph Muhozi**

KAMA inavyofahamika ni vigumu kwa mshumaa kudumu katikati ya kimbunga, aidha si rahisi kwa 'inzi' mwenye nia ovu kumsogelea kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un.

Jong- un vyombo vya habari vya magharibi vimekuwa vikimwelezea kwa namna ambayo imetofautiana sana na mtazamo wa Rais wa Marekani, Donald Trump na Mchezaji nguli wa Mpira wa Kikapu kutoka Marekani, Dennis Rodman' waliokutana naye uso kwa uso na kushiriki hafla mbalimbali.

Kiongozi huyu nchi yake hutengeneza makombora hatari ya nyuklia na imewahi kudaiwa kutishia usalama wa dunia kwa kumiliki makombora hayo. Lakini utetezi wake ni kwamba kama nchi ndogo inayotishiwa na Marekani na washirika wake, imeamua kutengeneza ngao ya kujilinda endapo itaguswa. Eti, ni kama wale wadudu wanaotoa harufu mbaya ukiwagusa, usipowagusa hiyo harufu hautaisikia hata wakipita mbele ya pua.

Kim Jong-un, ni mrithi wa kijiti cha uongozi kutoka kwa baba yake, Kim Jong-ill aliyefariki Desemba 17, 2011.

Hivi karibuni, waandishi wa Magharibi walisambaza taarifa za kufariki dunia. Rais Trump aliwapinga hakuamini taarifa hizo na kueleza kuwa kama zimetolewa na televisheni ya CNN hawezi kuwa na imani nayo. Na ukweli, ulithibitika kwamba kiongozi huyo yuko hai na ana afya njema.

Usiri wa maisha yake ni sehemu ya mbinu zinazotumiwa kumpa ulinzi mkali.

Hata vikosi vya majasusi vya CIA na FBI vya Marekani havina uhakika na umri wake ingawa amesoma Ulaya. Mwalimu mmoja aliyewahi kumfundisha Kim Jong-un nchini Uswizi, aliiambia BBC kwenye makala maalum kuwa 'anahisi' wakati huo alikuwa na umri wa miaka 14, ila hana uhakika. Hii ni kutokana na usiri wa maisha yake. Hivyo, wanakadiria kuwa atakuwa na miaka pengine 36 au 37.

> Makomando hao wanaopaswa kuwa na uwezo mkubwa wa kutumia silaha, kupigana mitindo ya 'martial art', hupewa mafunzo mengine maalum na makali ili kuwapa uwezo zaidi wa kipekee tofauti na makomando wengine katika kumlinda kiongozi wao.

### ULINZI WA KIPEKEE

Moja kati ya mambo yanayomtofautisha na viongozi wengi ni mtindo wa ulinzi wa kipekee, akiwa na walinzi 12 ambao huluzunguka gari lake na kukimbia nalo wakati wote wakihakikisha hakuna kinachomsogelea.

Walinzi hao ambao walionekana pia kwenye mikutano miwili ya awali kati ya Kim Jong-un na Rais wa Marekani Donald Trump, nchini Singapore na Hanoi, Vietnam, huvalia suti nyeusi na tai. Unaweza kujichanganya ukidhani ni 'waheshimiwa wabunge' kumbe ni makomandoo hatari.

Michael Madden, mkurugenzi wa taasisi rasmi inayofanya ufuatiliaji wa uongozi wa Korea Kaskazini (North Korea Leadership Watch), na mmoja kati ya wachambuzi wa masuala ya ulinzi wa viongozi, pamoja na vyanzo vingine anuai wamechambua uwezo wa walinzi hao na jinsi wanavyochaguliwa kati ya watu milioni 28.5 wanaounda Jamhuri ya Watu wa Korea.

Walinzi hao binafsi wa Kim Jong-un wanaokimbia pembeni mwa gari lake ni sehemu ya kikosi maalum kinachoitwa 'Central Party Office #6' au kwa jina rasmi 'The Main Office of Adjutants'.

Timu ya The Main Office of Adjutants huchaguliwa kutoka katika kikosi cha makomando wa Jeshi la Watu wa Korea Kaskazini (KPA).

Hata hivyo, pamoja na sifa ya kuwa makomandoo wenye uwezo wa hali ya juu, sifa nyingine muhimu hutazamwa katika kumchagua mlinzi wa kikosi hicho anayetakiwa kuwa pembeni ya kiongozi mkuu wa nchi ambayo iko kwenye mzozo mkubwa wa kijeshi na mataifa mengi yenye nguvu duniani, hususan Marekani na washirika wake.

### SIFA ZA KOMANDOO

Moja kati ya vigezo hivyo ni pamoja na kuangalia kimo cha komando anayechaguliwa. Huyu anapaswa kuwa na kima chenye uwiano unaoendana na kimo cha Kim Jong-un.

Pia, lazima komando anayechaguliwa awe na uwezo mzuri na usio na shaka wa kuona vizuri bila kutumia miwani.

Makomando hao wanaopaswa kuwa na uwezo mkubwa wa kutumia silaha, kupigana mitindo ya 'martial art', hupewa mafunzo mengine maalum na makali ili kuwapa uwezo zaidi wa kipekee tofauti na makomando wengine katika kumlinda kiongozi wao.

Hii inahusisha pia mafunzo ya kukwepa kunaswa na adui kwa namna yoyote na kuokoa mtu katikati ya maadui wenye silaha.

Kama ilivyo kwa makomando wengine, hupitia mafunzo ya uwezo wa mwili kukabiliana na mateso, mafunzo ya tabia na mengine. Lakini kwao huwa na ziada ya kutunza siri na hata kufa katikati ya mateso wakiilinda siri ya nchi yao. Msisitizo mwingine ni uwezo wa mlinzi huyo kutazama au kuona kwa haraka na kusoma eneo lote alipo kiongozi huyo, kubaini hatari na kusoma saikolojia za watu hata kwenye hadhara.

Hii ni tofauti kidogo na walinzi wengi wa wakuu wa nchi ambao huvaa miwani maalum myeusi yenye uwezo wa kuvuta taswira ya watu kutoka kwenye hadhara, kupiga picha na wakati mwingine kubaini vitu vya kielektroniki vinavyoweza kuwa tishio.

Lakini kwa walinzi hawa wa Kim Jong-un wao macho yao halisi yanatumika zaidi. Pamoja na uwezo huo, wana uwezo wa kuzima tishio 'lolote' kutoka kwa watu wa pembeni dhidi kiongozi huyo kwa kutumia mikono na miili yao, hata kama watu hao wana silaha.

Kati ya walinzi hao wanaokimbia wakitengeneza mzunguko kwenye gari, lazima awepo kiongozi mkuu wa kikosi hicho kutoka katika ofisi yao kuu kuhakikisha kila kitu kinaenda sawa, akiongoza na kuratibu kwa kushiriki moja kwa moja.

Hivyo, naye ni komando wa makomando mwenye mafunzo ya ziada anayefanya kazi kama maofisa wengine.

Ili kuhakikisha wanaaminika, walinzi hawa hufanyiwa uchambuzi wa hali ya juu wa familia zao na uzao wao, kwa kuangalia angalau vizazi viwili nyuma.

Hii hufanyika kwa maofisa wengi. Lakini, inadaiwa kuwa kwa Korea Kaskazini ufuatiliaji wa familia huchukua muda mrefu na uchambuzi huwa mkali sana. Hivyo, wafanyakazi wengi katika ofisi kuu ya ulinzi wake ni watu wenye uhusiano na familia ya Kim, au ni watu wa karibu wa familia za watu wenye nafasi za juu serikalini wanaoaminika.

Ofisi kuu ya ulinzi wa kiongozi huyo au 'Office of Adjutants' inaaminika kuwa na wafanyakazi kati ya 200-300 na zaidi ya nusu ya wafanyakazi hao ni makomandoo ambao ni walinzi wake binafsi, wengine ni madereva na wafanyakazi wengine.

Kazi yao kuu ni kumlinda Rais Kim Jong-un pekee. Kazi ya kuangalia usalama wa eneo alipo, chakula anachokula au vitu anavyotumia ni kazi ya kikosi kingine hatari kinachoitwa the 'The Guard Command' au the 'GC'.

### GUARD COMMAND

Kwa ufupi kikosi hiki cha The Guard Command au GC, ili upate picha ya tofauti ya kikosi cha walinzi wake wanaomwangalia yeye moja kwa moja na hiki ambacho kazi kubwa ni kuangalia maeneo aliyopo na vitu anavyotumia.

Kama umewahi kusikia inaelezwa kuwa 'kinyesi, mate au jasho' la Kim Jong-un hulindwa kwa gharama yoyote...basi hiki ndicho kikosi chenye kazi hiyo.

The Guard Command inahakikisha hakuna kitu chochote kinachodhuru kitakachomfikia kiongozi wao. Na pia, hakuna kinachotoka kwenye mwili wake kitakachoingia mikononi mwa adui au mtu asiyehusika.

**ITAENDELEA**

UCHAMBUZI

# Uchaguzi mkuu 2020 kinamama kubanwa na mifumo kandamizi?

**Na Gaudensia Mngumi**



Waziri wa Fedha wa Zanzibar, Amina Salim Ali. **PICHA: ZOTE MTANDAO.**




Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira.

BAADA ya pazia la Bunge la Bajeti kufungwa wakati wowote kuanzia sasa kitakachofuata ni kipenga cha mbio za ubunge, udiwani na urais, wanasiasa kuanza kujitosa majimboni kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa 2020.

Itakumbukwa kuwa mwaka 2015 wana CCM zaidi ya 10 waliibuka na kutangaza kusaka tiketi ya kuingia Ikulu kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba, ambao Rais John Magufuli, alichaguliwa kuliongoza taifa.

Aidha, itakumbukwa kuwa mchakato wa kujinadi wa mwaka huo ulichukua sura mbalimbali, wapo waliotangaza nia mbele ya kusanyiko kubwa, lakini wengine walichukua fomu kimya kimya, tena bila kujitangaza na wote walieleza kuwa nia yao ni kutumikia Watanzania.

Lakini, kwa mwaka huo, kilichojiri ni wanawake kutangaza nia rasmi na mmoja wa wagombea alikuwa Balozi Amina Salum Ali, ambaye alikuwa miongoni mwa waliojitokeza kifua mbele na kuandika historia.

Kukosekana wanawake wengi zaidi kwenye chama kikuu ni jambo lililojitokeza, lakini upinzani ulizidi 'kuwa doro' licha ya Ana Mghwira, kujitosa kugombea kupitia Chama cha ACT-Wazalendo.

Wanawake wanatajwa kuwa ndiyo wapigakura wakuu, lakini swali kubwa linabakia bila majibu wako wapi kwenye riadha ya kusaka tiketi za kugombea urais na ubunge? Ina maana wana nia kama wanaume lakini wanaogopa kutangaza kama kinababa wanavyofanya?

Kinachotafutwa ni kufahamu ni nini kinachowakwamisha kwenye ubunge na urais? Pengine fikra na maelezo yao ni kwamba huenda hawana fedha za kuwamwagia wapigakura na wajumbe wanaowapendekeza na kupitisha majina?

Licha ya Amina Salum Ali na Ana Mghwira kujitokeza ikumbukwe kuwa suala la mila na desturi za mfumo dume zinazohadaa kuwa wanawake hawawezi kuwa rais zimekuwa chanzo cha kuwarudisha nyuma.

Japo wanawake wanapotizama nyuma mwaka 2015 wanatiwa moyo na hatua ya Amina Salum Ali, kutangaza kuwa atagombea urais na kuchukua fomu.

Ni jambo lililostahili pongezi kwani haitawezekana kusema wanawake hawajajitokeza kwa vile walikuwapo, waliotangaza nia mapema na kuchukua fomu. Aidha, Ana Mghwira alikuwapo baada ya kupendekezwa na chama chake.

Hata hivyo, licha ya wawili hao kuonyesha nia swali linabakia kuwa kwenye umati wa wanaume hao watangaza nia na mbona kinamama ni wawili pekee waliojitokeza.

Kwa Tanzania ukiangalia wanawake ni wengi na ndiyo wapigakura kuwa zaidi tena si kwamba hawana sifa. Wanazo, lakini kumekuwapo na kusitasita kutokana na mifumo inayowafanya waogope kujitokeza.

Mifumo hiyo ya kitamaduni

> Licha ya Amina Salum Ali na Ana Mghwira kujitokeza ikumbukwe kuwa suala la mila na desturi za mfumo dume zinazohadaa kuwa wanawake hawawezi kuwa rais zimekuwa chanzo cha kuwarudisha nyuma.

inawabana, pia wanarudishwa nyuma na hofu ya kujitokeza, yote haya yanaleta kukosa uthubutu wa kuwania nafasi kubwa za uongozi kama na urais na ubunge majimboni.

### KUBANWA KIUTAMADUNI

Ni moja ya tatizo kwani kumekuwapo na desturi na imani kuwa wanaume ndiyo viongozi kwenye jamii. Licha ya kwamba hali hiyo haikubaliki na inakosolewa. Ndani ya vyama na serikali kuna sera, sheria, taratibu na miongozo ya kuinua wanawake kutokana na kuonewa, lakini hawajapewa nafasi ya kushiriki na kuwa sehemu ya kufanya maamuzi hivyo kunahitajika mikakati ya kuondoa mifumo hiyo.

Jamii kwa vile inaongozwa na mila na utamaduni kuna uwezekano wa kuchezewa rafu, kutukanwa matusi ya nguoni na wakati mwingine kudhalilishwa kwa hali ya juu.

Yote haya yanamfanya mwanamke kulazimika kujisafisha mara nyingi na kutumia muda na wakati wote kupinga madai ya kashfa na matusi na kejeli nyingi dhidi yake, hivyo anaona kuliko kufanya hivyo bora kuachana na kugombea ubunge au urais.

Pia, hakujawa na mikakati mahsusi ya kutekelezeka ya kuondoa kasoro hizo ambazo zimeendelea kuwarudisha nyuma wanawake.

Aidha, kuna hofu ya kuwaweka wanawake kugombea uongozi kwenye majimbo huenda wasichaguliwe.

Lakini, ukweli ni kwamba wanawake wanachaguliwa na wanapewa nafasi za kuongoza majimbo.

Kwa mfano mwaka 2015 wabunge wanawake kutoka majimboni wa Chadema walikuwa watano (mmoja amehama). Hii inathibitisha kuwa wanachagulika na wanakubalika ila kinachowakwamisha hawapewi nafasi.

### CCM IMETHIBITISHA

Kwa mfano mwaka 1995 kwenye uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi wanawake saba waliteuliwa na CCM ili kugombea ubunge kwenye majimbo.

Wote walishinda. Kadhalika mwaka 2000 walipitishwa 13 kuwania ubunge majimboni na 12 walishinda. Pia kwenye uchaguzi wa mwaka 2005 walikuwa 19 na waliochaguliwa ni 17.

Kwa mwaka 2010 waliopitishwa kugombea walikuwa 24 na waliopata ushindi ni 19. Hali hiyo inaonyesha kuwa wanawake wanachagulika na wanakubalika majimboni ila vyama haviwateui kugombea nafasi hizo.

Swali la kujiuliza ni hili katika majimbo zaidi ya 200 wanawake wangapi wanateuliwa na vyama vyao kugombea ikilinganishwa na wanaume?

Pengine vyama vinakosa mikakati ya kuwainua na kuwapa wanawake nafasi za kushiriki kwenye michakato ya kisiasa, japo si wanawake peke yao hata watu wenye ulemavu na makundi ya wanyonge. Kwa ujumla haviangalii suala la usawa wa kijinsia.

### SHERIA

Sheria kwenye vyama na nyingine zilizopo ni kikwazo kwa wanawake kwa vile hazivilazimishi vyama kuwa na asilimia au kiwango cha uwiano kinacholenga kuwa na safu yenye idadi sawa ya wanawake na wanaume kwa kiwango cha kulingana.

Hakuna sheria zinazotaka ndani ya vyama kufanya uteuzi unaozingatia uwiano wa wanawake na wanaume kwenye uteuzi wa wagombea wa serikali za mitaa, madiwani, wabunge na hata kwenye urais.

Licha ya kwamba katiba ya Tanzania inatambua suala la kuwa na viti maalumu ndani ya vyama, hakuna sheria za kuelekeza vyama kuwapitisha wanawake kuwa wagombea kwenye migawanyo mbalimbali ya mjukumu ya kiuongozi.

### KUHITAJIKA FEDHA

Tukirejea mwaka 2015 kukosekana wanawake kwenye mbio za kutangaza nia ya kugombea urais na hata ubunge huenda ni matokeo ya wasiwasi wa kukosa fedha kwa vile wengi uchumi wao ni mdogo.

Tatizo lililopo sasa ni uchaguzi kugeuzwa kuwa eneo la kutumia fedha kuanzia ngazi zote na kwa wanawake ni kikwazo kwa vile uchumi wao ni mdogo na hawana fedha za kujaza mifuko ya wapigakura na wajumbe wanaoshiriki kuwapitisha kwenye michakato hiyo.

Aidha, kukosekana kwao kwenye kinyang'anyiro si bahati mbaya kuona wanawake hawajajitokeza ni kitu kinachojulikana kwani vyama havina kanuni wala falsafa za kuwashirikisha wanawake kikamilifu.

Hata hivyo suala la nia na kugombea uongozi ni suala la uamuzi binafsi wa mwanasiasa.

Ni jambo linalotoka ndani ya moyo wa mtu hivyo si rahisi wengi wakawa na maamuzi hayo kutokana na sababu kadhaa lakini pia michezo michafu na rafu ndani ya siasa inaweza kuwa chanzo cha kuwakwamisha.

Wanawake ni viongozi wazuri na wenye maamuzi, lakini wanaangalia siasa kama eneo 'chafu' na wasingependa kujichafua na matope ya kisiasa.

# Yanayowadhalilisha wanawake kwenye uchaguzi yakomeshwe



Spika mstaafu, Anne Makinda, akiwa kazini bungeni. Ni mfano wa wanawake viongozi wanaodhihirisha kuwa kinamama wanaweza wakipewa nafasi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

DHANA ya usawa wa jinsia ni hali ya wanawake na wanaume kuwa na fursa sawa na kuwapo na haki zenye kuleta tija, katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya jamii, kati ya makundi hayo mawili.

Lengo kuu ni kutaka raia wote wawe na nafasi ya kukua na kuondolewa vikwazo mbalimbali ili wachangie na kutambuliwa kwa usawa katika maendeleo yao ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Hivyo, usawa wa jinsia katika ngazi mbalimbali za uamuzi na utekelezaji ni msingi muhimu kwenye maendeleo ya nchi na ndiyo maana wadau wa kutetea haki za wanawake wanapigania kuwapo na usawa huo.

Hata hivyo, wanaona kuwa kuna mambo kadhaa yanayokwamisha harakati zao za kutafuta nafasi za uongozi ili kuleta usawa wa kijinsia kwenye ngazi za uamuzi.

Wanataja baadhi ya mambo hayo kuwa ni rushwa ya ngono, fedha, khanga, fulana, kofia, chumvi na nguo za ndani, ambavyo wanadai hutolewa wakati wa mchakato wa kupata wagombea uongozi ndani ya vyama vya siasa.

Kwamba wapo baadhi ya wanasiasa ambao wako tayari kutoa vitu hivyo ili wachaguliwe, na kukwamisha harakati za wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi lakini hawana uwezo kifedha.

> "Kila tunapopata nafasi tunahimizana kupinga rushwa ya fedha, khanga, chumvi na vingine, badala yake wanawake wachaguliwe siyo wao kuwa wachaguaji tu.

Wakati huu ambao nchi inaelekea katika uchaguzi mkuu, wanawake wanahimizana wasikubali kubebwa katika kuwania nafasi yoyote badala yake wapitishwe au wachaguliwe kwa uwezo wao wa kuongoza.

Aidha, wanakumbushwa kuwa kukiwa na dalili za rushwa ya ngono au aina yoyote, basi wawasiliane na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), ili kupata msaada haraka.

Wanakumbushwa kuwa mwanamke hatakiwi kuteuliwa kwa rushwa ya ngono, bali kwa uwezo wake wa kuongoza, kwa kuwa uongozi ni sehemu ya haki yake, hivyo ajiamini na asikubali kubaishwa.

Hivyo ndivyo wadau wa kutetea haki za wanawake kutoka mikoa mbalimbali walikutana Dar es Salaam na kuazimia kuweka mikakati ya kuhamasisha ushiriki wa wanawake, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Ni hivi karibuni walipokutana na kujadili ushiriki wao katika uchaguzi mkuu, huku rushwa ya ngono, fedha na nyingine ikitawala mjadala ambao ulikuwa ukisimamiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Mwezeshaji wa majadala huo, Dk. Dinah Mbaga, ni Mshauri Mtaalam kutoka Tanzania Women Fund, anakiri kuwa jitihada za kuelekea usawa kwenye uongozi zimeanza kuonekana.

Lakini, anafafanua kuwa bado jitihada hizo zinahitajika zaidi ili kuhakikisha idadi ya wanawake na wanaume katika uongozi inakuwa sawa na kuondoa manung'uniko ambayo yamekuwapo kwa muda mrefu.

Kelele zao za kukemea rushwa zimeungana na za Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally ambaye hivi karibuni alikaririwa na vyombo vya habari akikemea rushwa ndani ya chama hicho.

Katibu huyo anakemea mtindo huo wa rushwa ndani ya chama chake unaofanywa na baadhi ya makada kwa kuwahonga wanachama vitu mbalimbali ili wawapendekeze kwenye kura za maoni.

Anawataka wajumbe wa vikao vya uteuzi ndani ya CCM wasikubali kununulika, kwa vile rushwa ni adui wa haki na kuongeza kuwa rushwa hiyo ya Sh. 5,000 na 20,000 ni ya dharau kwa wapigakura.

Anashangaa kusikia baadhi ya wanachama wakizunguka na sukari na vitenge na Sh. 5,000 au 10,000 kwa lengo la kuhonga wajumbe, na kwamba hiyo ni dharau na matusi kwa wapigakura akiwataka waache.

Katibu huyo anahoji kama mtu ana sifa kwa nini ahangaike kujipaka wanja, na kwamba anatakiwa kujua kwa CCM haitafuti mrembo bali kiongozi bora, na kuwataka makada wenye mchezo huo waache.

Kwa kauli hiyo, Dk. Bashiru atakuwa amewakuna wanaharakati za kutetea wanawake wakiwamo Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGP) ambao wanakemea vitendo vya kuwahonga wanawake ili watoe kura zao.

Wanawake wanaamini kwamba huo ni udhalilishaji dhidi yao, na wanawataka wahusika waache mara moja na pia hawataki kuendelea kuwa wapigakura tu bali wachaguliwe katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Wanaamini kwamba ushirikishwaji wa wanawake katika shughuli za kimaendeleo bado unahitaji msukumo zaidi ili kuwajenga katika kujikomboa badala ya kutumika tu.

Kwa vile wamekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha wanawake wengi zaidi wanateuliwa au wanachaguliwa kwenye nafasi mbalimbali za uongozi, kauli ya Dk. Bashiru itakuwa umegusa pale wanapopataka.

**WANACHOAMINI WADAU**

Wadau wa utetezi wa wanawake wanasema, katika uchuguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2014, idadi ya wanawake waliochaguliwa kuongoza mitaa, vijiji na vitongoji ilikuwa ndogo ikilinganishwa na wanaume.

Kwamba hali halisi ya ushiriki wa wanawake katika uongozi bado uko chini ikilinganishwa na ushiriki wa wanaume, kama ripoti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) ya uchaguzi wa serikali za mitaa ya mwaka 2014 inavyoeleza..

Katika uchaguzi huo wenyeviti wa mitaa, wanasema waliochaguliwa walikuwa ni 3,929, kati yao wanawake wakiwa ni 435, na waliochaguliwa nafasi za mwenyekiti wa vijiji ni 12,275, kati yao wanawake wakiwa ni 223.

Nafasi ya wenyeviti wa vitongoji, Tamisemini inaeleza kuwa waliochaguliwa ni 64,691, kati yao wanawake wakiwa ni 3,482 tu, na kwamba idadi hiyo ni ndogo na bado wanasubiri taarifa ya uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka jana.

Msisitizo wao upo katika kukemea rushwa, kwamba yakikoma, basi wanaweza kupenya kwa wingi kwenye uchaguzi mkuu ujao iwapo watakuwa wamechukua fomu kuwania uongozi.

Wanaamini kwamba hicho ndicho chanzo cha kuwafanya wawe nyuma huku baadhi yao wakiwa hawajui haki zao na kujikuta wakishawishiwa na kukubali kutumika bila wao kujua.

"Kila tunapopata nafasi tunahimizana kupinga rushwa ya fedha, khanga, chumvi na vingine badala yakee wanawake wachaguliwe siyo wao kuwa wachaguaji tu," anasema Lilian Liundi, Mkurugenzi Mtendahji wa TGNP.

Anaongeza kuwa, iwapo wanaosaka uongozi kwa rushwa wataacha ili mchakato uchukue nafasi, wanawake wengi zaidi wanaweza kupenya na kupata nafasi za uongozi na hatimaye kufikisha 50 kwa 50 ambayo wamekuwa wakiitaka.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**Anahitajika** mtu mwenye elimu ya Usimamizi wa miradi au Project officer. Kwa mawasiliano Piga simu 0716 172929 au 0786 641903


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**
**Mahakama ya Mwanzo ya Mjini**
**Wilaya ya Nachingwea**

**MADAI NAMBARI 8 YA 2020**
**Mdai Rogers William Njole**

Kwa: DAYANA PETER
ARUSHA

Kwa kuwa Mdai/Wadaiwa yake/wao kwamba/Elezea hapa ya mdai): Unashauriwa na Mahakama hii ufike bila kukosa kuja kusikiliza Shauri hili la Madai.

Kwahiyo unahitajika/mnahijika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya: Jumatatu tarehe 25/05/2020 saa 2.00. Asubuhi/Alasiri kwa kujibia Madai hayo na shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku hiyo ilitajwa hapo juu, Mahakakama ikithibitiwa kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo.
Tarehe 12/05/2020

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi Na. 105/2020
Ombi la **REHEMA HOSIANA MWAKATUMBULA** kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **HOSSIANA CHARLES MWAKATUMBULA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 27/05/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 27/04/2020.

Sahihi ya Hakimu

157391

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA**
**MBEYA**
**SHAURI NO.139/2019**
**SIMON JULIUS GATUNA::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**

| | | |
|---|---|---|
| RICHARD JACKSON | SHINA TAMSON | SILIMA MAJALISI |
| SILINJANJE ZAMBI | JACKSON WILSON | MESIYA SIMKONO |
| E.MWAKALANDILE | CHARLES MWAKAMBONJA | SHOGO TAMSON |
| LYEGO JACKSON | SAMLI MWALYOBELO | MAJALIWA MWAJOBELO |
| HOYE MWASAKA | FRANK ADAM | SHAKA WILSON |
| NDUNDU TAMSON | MARY JACKSON | MALUGU BOYMANDA |
| DANIEL NJANGO | JOSIA LAMECK | ISMAIL MWINUKA |

Fahamu kwamba Simon Julius Gatuna amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 19/05/2020 saa2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza,mnatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya tangazo hili.

Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba ya wilaya ya Mbeya.

Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza sikuhiyo bila kukosa ninyi wenyewe au wawakilishi wanaoruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.

Kumbuka:Musipo hudhuria siku ya baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo ninyi kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 27/04/2020.

T.Munzerere
Mwenyekiti

157387

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA**
**MBEYA**
**SHAURI NO.139/2019**
**SIMON JULIUS GATUNA::::::::::::::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**

| | | |
|---|---|---|
| LAURENT LAITON | JASON WILSON | CHAKUPEWA KIBASI |
| PRISCA MAJALISI | LANGSON MANAWLI | ARNOD MWALYOYO |
| ROZINA VYASYOLE | KASSIM TALA | JUMANNE NJANGO |
| UPENDO MAJALIWA | SHEYO VYASOLE | KENNEDY SAWANGA |
| PATRISIA EKISAUDI | CHRISTINA NZALA | HERMAN MACHUMA |
| BELITA SAMLI | JULIUS SAMLI | MARY VYASOLE |
| DICKSON MWATUMBE | MASHAKA | EVANS SHEYO |

Fahamu kwamba Simon Julius Gatuna amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 19/05/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza mnatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya tangazo hili.

Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Aridhi na Nyumba ya wilaya Mbeya.

Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa ninyi wenyewe au wawakilishi wanaoruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.

**Kumbuka:**Musipo hudhuria siku ya ya baraza litatoa stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo ninyi kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 27/04/2020.

T.Munzerere
Mwenyekiti

157387

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;116/2020
Ombi la AMINA J.MLANDA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ERICK CHRISTOPHER KABWOGI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/05/2020.

Sahihi ya Hakimu

157386

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI-MOROGORO**
Usimamizi wa mirathi **No;117/2020**
Ombi la IZACKIEL MARTIN Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu CONSOLATA BONIFACE CANCEL
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/05/2020.

Sahihi ya Hakimu

157385


***NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# NSSF yatangaza bei nyumba za Kigamboni

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limetangaza bei ya nyumba zake zilizopitishwa na mthamini mkuu wa Serikali kuwa kodi ni kati ya Sh. 250,000 hadi 500,000.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, akizunguma hivi karibuni alipotembelea nyumba za Kigamboni na Dungu Jijini Dar es Salaam, alisema wateja wataruhusiwa kulipa kwa mwezi, miezi mitatu na mwaka mmoja kutegemea na aina ya nyumba.

Alisema katika mradi wa Dungu nyumba zilizokamilika ni 99, kati yake 59 zimeshapangishwa, nyumba 10 zimekabidhiwa kamati ya ulinzi na usalama Wilaya ya Kigamboni na 16 zimekabidhiwa wakuu wa idara za Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni, na kwamba zimebaki 15.

Mpangaji anatakiwa kulipa kiasi hicho cha fedha na Sh. 100,000, kwa ajili ya gharama za uendeshaji," alisema.

Naye, Meneja wa Miliki wa NSSF, Augustino Paul, aliwataka wananchi kuchangamkia nyumba zilizoko Kigamboni na Tuangoma, ambazo bei zake ni nzuri kwenye kupangisha.

Alisema NSSF ina nyumba 76 zilizoko Toangoma ambazo zinauzwa na kupangishwa kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Paul, nyumba hizo zinapangishwa kati ya Sh. 350,000 na 400,000 kwa mwezi, na kwamba nyumba 33 za Mtoni Kijichi zinazopangishwa kati ya Sh. 400,000 na 500,000.

Aidha, alisema nyumba zote ni za kisasa na zina huduma zote, na kwamba wananchi wote wanakaribishwa kuchangamkia fursa hiyo.

**Katika mradi wa Dungu nyumba zilizokamilika ni 99, kati yake 59 zimeshapangishwa, nyumba 10 zimekabidhiwa kamati ya ulinzi na usalama Wilaya ya Kigamboni na 16 zimekabidhiwa wakuu wa idara za Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni, na kwamba zimebaki 15.**

# Waziri akabidhi injini za mil. 320/- kwa wavuvi

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amekabidhi injini 73 za boti za uvuvi zenye thamani ya Sh. milioni 320 kwa ajili ya kusaidia vikundi vya ushirika wa wavuvi katika maeneo mbalimbali nchini.

Akikabidhi injini hizo kwa Wabunge Makao Makuu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mtumba mjini Dodoma, Waziri Mpina alisema kati ya injini hizo 73 serikali imegawa bure injini 13 zenye thamani ya Sh. milioni 60 kwa ajili ya kusaidia vikundi vya ushirika wa wavuvi.

Waziri Mpina alisema injini nyingine 60 zenye thamani ya Sh. milioni 260 zimetolewa kwa ruzuku ya serikali ambapo wavuvi wamechangia asilimia 60 na serikali imechangia asilimia 40 kama sehemu ya kuwezesha ukuaji wa sekta ya uvuvi.

Wakizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mbunge wa Kyela na Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alimshukuru Mpina kwa kuamua kuwasaidia wavuvi vifaa vya kisasa vya kuvulia na kwamba vitaleta tija kubwa kwa wavuvi wa Ziwa Nyasa.

Naye Mbunge wa Mtwara Vijijini, Hawa Ghasia, alisema msaada wa serikali kwa wavuvi mara ya mwisho ulitolewa wakati Rais John Magufuli alipokuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, hivyo kumshukuru Waziri Mpina kwa uamuzi huo wa kuwakumbuka na kuwasaidia zana za kisasa wavuvi.

Mbunge wa Ukerewe, Joseph Mkundi, alisema msaada huo umekuwa wakati mwafaka na kuonyesha serikali inathamini maendeleo ya uvuvi tofauti na dhana iliyojengeka hapo awali kwamba serikali kazi yake ni kukamata tu wavuvi kwa zana haramu.

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama, alisema msaada huo utakuwa chachu ya mabadiliko ya wavuvi katika Wilaya ya Kaliua, na kwamba wilaya hiyo itahakikisha vifaa hivyo vinatunzwa ili viweze kuleta matokeo chanya yaliyotarajiwa na serikali.



Fundi Said Mwandike, akitengeneza vyombo vya kulishia mifugo kwa ajili ya kuuza ili ajipatie riziki, katika Soko la Vetenari, Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wajawazito wawekewa utaratibu kuwakinga na virusi vya corona

Na Pendo Thomas, KIGOMA

WAJAWAZITO mkoani Kigoma wametakiwa kuendelea kuhudhuria kliniki kama walivyopangiwa na wataalamu wa afya katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona, kwa kuwa utaratibu wa kuwakinga dhidi ya ugonjwa huo wanapopatiwa huduma ushafanyika.

Akielezea hatua mbalimbali zilizochukuliwa na mkoa huo ili kulinda kundi linaloenda kupata huduma za afya ya uzazi, Mratibu wa afya ya uzazi na mtoto mkoani hapo, Ernest Teyumwete, alisema vituo vya kutolea huduma vimeweka utaratibu wa kutoa huduma kwa mtu mmoja mmoja tofauti na utaratibu ule wa awali uliokuwa ukiwakusanya kwa pamoja.

Pia Teyumwete alieleza wameongeza saa na siku za kutoa huduma hizo ili kuondoa msongamano katika maeneo ya kutolea huduma ya kliniki ya baba, mama na mtoto kwa kuwa kama kituo kilikuwa kinatoa huduma hiyo kwa siku tatu kwa wiki kwa sasa kinalazimika kutoa kwa siku tano na zaidi.

"Sisi kama watoa huduma tumejipanga kuhakikisha tunatoa huduma tena kwa wakati bila kusababisha msongamano hivyo wananchi wasitumie kisingizio cha ugonjwa huo kutokwenda kliniki," alisema.

Mmoja wa watoa huduma katika kituo cha afya cha Ujiji, kilichoko katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, Leonida Leonard, alisema kwa sasa hakuna msongamano kwa kuwa wanahudumia mtu mmoja mmoja na kwa siku moja wanahudumia watu 18 hadi 20.

Juma John, aliyemsindikiza mke wake kliniki alisema baada ya kufika kituoni hapo amejionea taratibu na namna huduma zinavyotolewa kuwa zinalinda kundi la wanaopata huduma ya afya ya uzazi kuwa salama hivyo wananchi waendelee kuhimizana kwenda kupata huduma.

"Mimi nimemleta mke wangu hapa kliniki ni mjamzito mazingira ya huduma ni ya tahadhari sana hivyo watu wengine wasiogope kuja ili kuendelea kufahamu maendeleo ya ujauzito," alisema.




# COURTOIS AFAFANUA UBINGWA MADRID

**MADRID,** Hispania

THIBAUT Courtois amefafanua kauli yake kuhusu Barcelona, akisema kamwe hakutamka Real Madrid inatakiwa kupewa ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, msimu huu.

Golikipa huyo wiki iliyopita alisema kwamba, Barca hawapaswi kupewa ubingwa kama msimu huu utafutwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Lakini wakati msimu wa LaLiga ukipangwa kumaliziwa vijana wa kocha Quique Setien wanaongoza kwa tofauti ya pointi mbili dhidi ya Madrid, huku kukiwa kumebakiwa na mechi 11 za kuchezwa.

Courtois amelezea kauli yake na kusema kwamba, hakuwa na maana kwamba Madrid wapewe ndoo hiyo.

"Kwa hakika kabisa sikusema kwamba, Real Madrid wanapaswa kupewa ubingwa," alisema katika mahojiano na televisheni Espanola.

"Kama ligi itamalizwa, tupo kwenye nafasi nzuri hata kama tulifungwa na (Real) Betis.

"Kama tukicheza mechi 11 zilizobaki, ninaamini timu yangu inaweza kushinda taji la Ligi Kuu."

Courtois alianza mazoezi Jumatatu huku ligi hiyo ya LaLiga ikitarajiwa kurudi tena Juni.

Raia huyo wa Ubelgiji alikuwa na furaha kurudi tena mazoezini, baada ya kusimama kwa muda mrefu kutokana na mlipuko wa virusi vya COVID-19.

"Lilikuwa jambo zuri kurudi kwenye mazoezi," alisema Courtois.




# Barcelona na Inter wamalizana kwa Martinez

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona inaonekana imekaribia kumnasa mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia pale Camp Nou, ambako anaweza kucheza na mchezaji mwenzake wa timu ya taifa, Lionel Messi.

Makubaliano yanaonekana yamekwishafikiwa kati ya Inter na Barcelona kwa ajili ya usajili wa Martinez.

Barcelona na Inter kwa sasa wapo katika hatua ya mwisho ya kumalizana kuhusu dili hilo la Martinez, kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

Ripoti hiyo inasema kwamba klabu hizo mbili zimefikia makubaliano ya euro milioni 60 pamoja na kuwatoa viungo wawili kati ya Arturo Vidal na Nelson Semedo au Emerson.

Sky Sport Italia pia imeripoti Barca na Martinez wameshafikia makubaliao ya maslahi binafsi na atasaini mkataba wa miaka minne.

# Cannavaro: Messi? Hakuna kama Iniesta

**ROME,** Italia

FABIO Cannavaro ameeleza kumhusudu Andres Iniesta, akisema amemwangalia zaidi kiungo huyo wa zamani wa Barcelona kuliko Lionel Messi.

Iniesta, kwa sasa anacheza Ligi Kuu ya Japan, J1League, katika klabu ya Vissel Kobe na Jumatatu wiki hii alisherehekea kutimiza umri wa miaka 36.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Hispania, aliondoka Barcelona mwaka 2018 baada ya kuwa na mafanikio ya kuvutia kwa mabingwa hao wa LaLiga.

Cannavaro, ambaye alishinda mataji mawili ya LaLiga akiwa mchezaji wa Real Madrid, amesema mara zote macho yake yalikuwa kwa Iniesta, akimtaja kama mmoja wa viungo bora wa wakati wote duniani.

"Anacheza kwa staili ya kuvutia mno, unachoweza kufanya ni kumpenda tu kwa namna anavyocheza," alisema Muitaliano huyo akinukuliwa na gazeti la AS.

"Alikuwa mchezaji wa kiwango cha juu kabisa na mnyenyekevu...nilimpenda sana.

"Kila mmoja anaweza kuwa anamwangalia Messi, lakini mimi nilikuwa namwangalia zaidi





# LAPORTA KUMRUDISHA GUARDIOLA BARCELONA

**BARCELONA,** Hispania

JOAN Laporta anapanga kuingia kwenye uchaguzi wa urais wa Barcelona mwakani na anataka kumrudisha Pep Guardiola kama akifanikiwa kushinda.

Laporta alitumia miaka saba kama rais wa Barca kabla ya kujiuzulu mwaka 2010.

Muongo mmoja baada ya kuondoka madarakani pale Camp Nou, Laporta mwenye umri wa miaka 57, sasa anataka kumrithi Josep Maria Bartomeu mwaka 2021.

Laporta alimpandisha Guardiola aliyekuwa hana uzoefu katika kikosi cha kwanza mwaka 2008 na akafanya makubwa.

Kama Laporta akishinda uchaguzi huo, kocha huyo wa sasa wa Manchester City atakuwa njiani kurejea Catalunya.

Ameiambia televisheni ya Katalunya, TV3: "Nafanya kazi ya kujitambulisha mimi mwenyewe kama mgombea wa urais.

"Nilikuwa rais kabla na nina hamasa ya kutaka kurudi tena. Hali halisi mwaka 2021 itakuwa ya kuvutia na nahitaji kufanya kazi. Nafanyia kazi kwa watu ninaowaamini."

Aliongeza: "Ningependa kumrudisha Guardiola, lakini sasa yupo pale City na utakuwa uamuzi wake."

# *Coutinho kumaliza msimu na Bayern Munich*



**MUNCICH,** Ujerumani

HANSI Flick bado anamatumaini Philippe Coutinho anaweza kuwa na mchango mkubwa kwa michezo iliyobaki ya Bayern Munich, baada ya kuripotiwa kwamba atakaa nje kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki.

Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, imepanga kuwa ligi ya kwanza barani Ulaya kurudi kumalizia msimu baada ya kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Kiungo huyo wa Bayern, Coutinho alifanyiwa upasuaji Aprili 24, mwaka huu kwenye kifundo cha mguu wa kulia na ilibainishwa atakaa nje kwa kipindi cha wiki mbili.

Hata hivyo, nyota huyo anayecheza kwa mkopo hapo Bayern akitokea Barcelona, aliripotiwa kwamba hangeweza kurudi dimbani kwa msimu huu, na amekuwa akihuishwa na mpango wa kuondoka hapo.

Lakini Flick bado ana matumaini kwamba, Coutinho anaweza kucheza katika mechi zilizobaki za Bayern.

"Pengine anaweza kucheza katika mechi za mwisho," alisema kocha huyo akiliambia gazeti la Kicker.

# Pirlo: Siwezi kumfikia Tonali

**ROME,** Italia

KIUNGO mkongwe Andrea Pirlo amepuuzia maneno ya kulinganishwa na Sandro Tonali, akisema nyota huyo wa Brescia ni "kiungo aliyekamilika zaidi kuliko yeye".

Tonali amekuwa akihusishwa na miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus na Inter baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia kule Brescia, huku akiichezea kwa mara ya kwanza timu ya Taifa ya Italia mwaka jana.

Kinda huyo mwenye umri wa miaka 20, amekuwa akilinganishwa sana na mkongwe wa Italia, Pirlo, lakini gwiji huyo wa zamani wa Juventus na Milan anaamini Tonali anaweza kuwa bora zaidi kuliko yeye.

"Wanasema kwamba pengine ndiye mrithi wangu, lakini sioni vitu tunavyofanana," alisema akimuambia Nicolo De Devitiis wakati wa mahojiano live kupitia Instagram.

"Ni aina tofauti kabisa ya uchezaji wake. Yeye amekamilika zaidi na ana uwezo wa kushambulia na kulinda, hivyo ana nafasi kubwa zaidi ya kuwa bora kuliko mimi.

"Ni mchezaji kijana ambaye kwa sasa anaongelewa sana Italia na barani Ulaya, namuona ni kiungo atakayekuwa na mafanikio makubwa mno hapo baadaye."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CANAVARRO: MBAPPE APEWE VIATU VYA CR7

●●● Asema wanataka mchezaji kijana, lakini watapata tabu sana...

**MADRID,** Italia

FABIO Cannavaro anaamini Real Madrid wanamhitaji Kylian Mbappe ili kufuata nyayo za Cristiano Ronaldo, lakini anahisi watapata tabu sana kumsajili nyota huyo wa Paris Saint-Germain.

**Mbappe mwenye umri wa miaka 21, ameendelea kuhusishwa na mpango wa kuhamia Madrid kutoka PSG, ambako ameng'ara kwa kipindi cha misimu mitatu.**

Madrid imekuwa kwenye wakati mgumu kupata mrithi wa Ronaldo, ambaye aliamua kuondoka kwa miamba hao wa LaLiga na kujiunga na Juventus mwaka 2018.

Cannavaro, ambaye alishinda mataji mawili ya LaLiga wakati akiwa anaichezea Madrid, amesema Mbappe anaweza kuwa mchezaji ambaye klabu hiyo inamhita kufuata nyayo za Ronaldo.

"Real Madrid inahitaji mchezaji kama Mbappe, nyota kijana ambaye anaweza kufuata nyayo za Cristiano Ronaldo," alisema kocha huyo wa timu ya Guangzhou Evergrande akinukuliwa na gazeti la AS.

"Ni kawaida kwamba Madrid wanataka kumsajili yeye, lakini pia lazima ikumbukwe kua mmiliki wa PSG anahitaji fedha. Na malengo yao wanataka kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nafikiri itakuwa ngumu kwa Madrid kumpata. Rais wa PSG ni mtu ambaye anataka kushinda, nawajua wao vizuri tu na wanapigana kwa jino na msumari kumbakiza Mbappe."

Mbappe ambaye ameshinda Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, ni pia ametwaa taji moja la Ligue 1, Coupe de France na Coupe de la Ligue akiwa na PSG.

Amefunga mabao 30 katika mechi 33 katika mashindano yote msimu huu, wakati Ligue 1 ilipofutwa kwa mlipuko wa virusi vya corona.

## ZISIKUPITE

### OZIL HAONDOKI ARSENAL

NYOTA wa Arsenal, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 31, hataondoka katika klabu hiyo msimu huu na badala yake atakamilisha mwaka mmoja uliobaki katika mkataba wake na 'Washikabunduki' hao. ***(Fanatik)***

### LEIPZIG VITANI EVERTON BARCA

RB Leipzig wameungana na Everton katika kinyang'anyiro cha kumsaka beki wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 20, Jean-Clair Todibo kutoka Barcelona. ***(HITC)***

### UNITED KWA MUARGENTINA

KLABU ya Manchester United inataka kumsaini kiungo wa Argentina, Thiago Almada mwenye umri wa miaka 19, ambaye pia ananyatiwa na Arsenal. ***(Tutto Mercato)***

### CEBALLOS KUFUNGWA

KLABU ya Arsenal ina matumaini ya kubakisha kiungo wa kati wa Real Madrid, Dani Ceballos mweye umri wa miaka 23, kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu huu, lakini wanapanga kurefusha mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania kwa msimu mmoja zaidi. ***(El Confidencial)***

### GOMES MKATABA BADO UTD

MANCHESTER United bado hawajakubaliana kuhusu mkataba mpya na kiungo wa kati, Angel Gomes mwenye umri wa miaka 19, ambaye mkataba wake wa sasa unakamilika mwisho wa Juni. ***(Goal)***

### MAHREZ CHUPUCHUPI LIVER

WINGA wa kimataifa wa Algeria, Riyad Mahrez mwenye umri wa miaka 29, amesema Liverpool walitaka kumsajili kabla ya kujiunga na Manchester City akitokea Leicester City, lakini 'Wekundu' hao walisitisha mpango huo walipompata Mohamed Salah kutoka AS Roma. ***(Bein Sports)***

### CHELSEA YATUA DORTMUND

KLABU ya Chelsea inaamini itampata, Charlie Webster, ambaye anaripotiwa kunyatiwa na Borussia Dortmund, mara tu atakapofikisha umti wa miaka 17, Januari mwakani. ***(Telegraph)***

### JUVE WAKOMAA NA POGBA

KLABU ya Juventus bado inaangalia uwezekano wa kumsajili nyota wa Manchester United, Paul Pogba na pia wapo tayari kuwatoa wachezaji wawili, Aaron Ramsey na Adrien Rabiot ili kukamilisha dili hilo. ***(AS)***

### PJANIC TAYARI KUTUA BARA

MAZUNGUMZO juu ya Miralem Pjanic kuondoka Juventus na kujiunga na Barcelona yamefikia pazuri, baada ya mimba hao wa Italia kuikubali ofa ya klabu hiyo kutoka Katalunya. ***(Sport)***

### DEMBELE ANGA ZA UNITED

NYOTA wa Lyon, Moussa Dembele anaendelea kuzivutia klabu za Ligi Kuu ya England. Kwa mujibu wa taarifa kutoka England, klabu ya Manchester United ndio inyoongoza katika mbio za kuinasa saini ya mshambuliaji huyo ambaye thamani yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 60. ***(Daily Star)***

HABARI MICHEZO

## Mbeya City yalilia kikao klabu, TPLB

**Na Faustine Feliciane**

KATIBU Mkuu wa Klabu ya Mbeya City, Emmanuel Kimbe, amesema Bodi ya Ligi (TPLB) inapaswa kuitisha kikao na klabu zote kujadili mustakabali wa Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza.

Kimbe (pichani chini) amesema serikali imeonyesha nia ya kuruhusu michezo kuendelea baada ya kusimama kutokana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona, lakini ni lazima kikao cha pamoja kifanyike kujadili namna bora ya kuendesha ligi kwa michezo iliyobakia.

"Ni lazima na sisi kama klabu tutoe maoni yetu namna ya kumalizia michezo iliyobakia wakati huu ambapo tunajua serikali imeonyesha nia ya kuruhusu michezo iendelee," alisema Kimbe.

Aidha, alisema ligi itakaporejea ni vyema ikaendelea katika utaratibu ule ule wa kucheza mechi nyumbani na ugenini.

" Haya yanaweza yakawa maoni yangu, lakini kwa sababu ya janga linalotukabili ni vema sisi kama klabu tukakutana na Bodi ya Ligi na kuangalia namna nzuri zaidi," alisema.



## Sababu makipa Zanzibar kuvurunda

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUFUNZI wa Makocha wa Magolikipa, Salehe Machupa amesema changamoto kubwa inayosababisha kukosa magolikipa wenye viwango hapa nchini ni klabu kutoajiri makocha wa makipa.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema klabu bado hazijakubali kuona umuhimu wa kuajiri makocha wa magolikipa hali inayosababisha kushindwa kupatikana magolikipa wenye viwango kuendana na soka la sasa.

"Suala la kupata makipa wa viwango, lazima Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) ichukue maamuzi magumu ya kuhakikisha kila timu inakuwa na makocha wa magolikipa ikilinganishwa na hivi sasa ambapo ni klabu chache tu ambazo zina makocha hao, utakuta timu kama inamakipa watatu basi mazoezini wanarushiana mipira wenyewe kwa wenyewe pasipo kuwa na walimu maalum wa kuwafanyisha mazoezi, kwa staili hii hatuwezi kupata makipa bora," alisema.

Aidha, alisema changamoto hii ya makipa inasababisha hata kukosa soko la makipa kucheza klabu nje ya Zanzibar kama ilivyo kwa wachezaji wa nafasi za viungo na washambuliaji.

# HITIMANA: NAMUNGO IPO VIZURI, LIGI KUU NA IREJEE

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI makocha wakisikilizia siku rasmi ya kurejea kwa Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Klabu ya Namungo FC, Mnyarwanda Hitimana Thierry ameahidi kikosi chake kurudi na ushindani wa hali ya juu pindi Ligi Kuu itakapoanza kurindima tena nchini.

**Ligi Kuu Bara ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), lakini Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, Mei 3, mwaka huu akiwa Chato mkoani Geita alisema anafikiria kuruhusu ligi za soka nchini kuendelea na anachosubiri ni kupata ushauri kutoka kwa wataalamu wake.**

Kauli hiyo ya Magufuli, ililipa nguvu Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB), ambayo ilitangaza kuwa endapo itapata baraka za serikali ligi hiyo itarejea mapema Juni mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe kutoka nchini Rwanda, Hitimana alisema hana wasiwasi na wachezaji wake kutokana kuwa na nidhamu pamoja na umakini waliokuwa nao kabla ya ligi hiyo kusimama.

"Nipo tayari muda wowote kurudi uwanjani kuendelea na michezo iliyobaki kama serikali itaturuhusu ili kuipa timu yangu nafasi nzuri," alisema kocha huyo ambaye ameifanya Namungo kuwa miongoni mwa timu tishio msimu huu ambao ni wa kwanza kwao kucheza Ligi Kuu.

Hadi ligi hiyo inasimama, Namungo ipo nafasi ya nne kwenye msimamo ikiwa na alama 50 baada ya mechi 28, ikizidiwa pointi nne na Azam FC inayoshika nafasi ya pili na alama moja dhidi ya Yanga yenye mechi moja mkononi, wakati huu Simba ikiwa kileleni na pointi 71.

Akizungumzia mafanikio hayo, Hitimana alisema siri kubwa ni ushirikiano mzuri uliopo kati ya uongozi pamoja na wachezaji.

"Siri ya sisi kufanya vizuri ni ushirikiano mzuri uliopo kati yetu na wachezaji jambo ambalo linanipa matumaini makubwa," alisema.

Alisema atapambana kwa nguvu zote kuhakikisha klabu hiyo inashika nafasi nzuri katika msimamo wa Ligi Kuu, licha ya kuwapo kwa ushindani mkubwa.

"Ligi inaushindani mkubwa jambo linalomfanya kila mchezaji afanye juhudi anapokuwa anapewa maelekezo na mwalimu wake akihofia kukosa nafasi katika kikosi cha kwanza," aliongeza.

TULIA IJE TU...



Wanariadha wa timu ya Mkoa wa Dar es Salaam wakifanya mazoezi katika viwanja vya nje vya Taifa jana, kwa ajili ya maandalizi ya mbio za Tulia Ackson zitakazofanyika Agosti mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Azam tayari kwa lolote Ligi Kuu*

**Na Saada Akida**

MTENDAJI Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', amesema wapo tayari kwa maamuzi yoyote serikali itakayotoa kuhusu utaratibu utakaotumika endapo itabariki Ligi Kuu Bara kurejea.

Kauli hiyo ya Popat inatokana na kuwapo maoni tofauti kutoka kwa wadau wa soka wengine wakipendekeza ligi hiyo ichezwe katika kituo kimoja na bila mashabiki, huku baadhi wakitaka muundo wa awali wa nyumbani na ugenini urejewe na watazamaji wachache waruhusiwa kuingia uwanjani.

Popat ameliambia gazeti hili jana kwamba, kwa upande wao Azam FC wanasubiri tamko la serikali na Bodi ya Ligi (TPLB) juu ya ligi hiyo kuchezwa kwa muundo upi.

Alisema endapo itachezwa kituo kimoja au bila ya mashabiki kwao wanaona ni sawa tu kutokana na uwapo wa janga hilo la corona.

"Hili janga bado lipo, ni dunia nzima, hivyo kwanza usalama wa watu, hivyo kama maamlaka watatoa maamuzi ya ligi ichezwe katika kituo kimoja ama nyumbani na ugenini pia bila mashabiki kwa upande wetu tunalipokea," alisema.

Popat alisema ligi kuchezwa bila mashabiki ni mtihani mkubwa ila wana imani hii ni dharura ambayo imejitokeza na hawana budi kukubaliana na hali halisi.

"Hivi sasa tunawasisitiza wachezaji wetu kujikinga pia kufanya mazoezi kwa maelekezo ya programu waliyopewa na mwalimu, kujiweka fiti kwa sababu hatujajua lini tutarejea uwanjani," alisema mtendaji huyo.

Azam ipo katika nafasi ya pili ya msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 54, wakati huu Simba ikiwa kileleni na pointi 71 baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 28, huku Yanga iliyopo mechi moja nyuma ikiwa na alama 51 katika nafasi ya tatu.

Michezo
Jumatano Mei 13, 2020
Nipashe



Canavarro: Mbappe apewe viatu vya CR7 UKURASA 22

SUBIRINI...



Kiungo wa Simba, Ibrahim Ajibu, ambaye anahusishwa na kutakiwa na timu nyingi za nje ya nchi, akiwa katika moja ya mazoezi ya timu yake msimu huu. **PICHA: MAKTABA**

# Ajibu si wakuichezea tena Yanga- Meneja

## ●●● Asema ofa kibao kutoka nje zimemshukia, waiachia Simba iamue kwa sababu...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kutopewa nafasi ya kutosha katika kikosi cha kwanza cha Simba, Ibrahim Ajibu si mchezaji wa kucheza tena soka nchini hata kama Yanga ama Azam FC zitahitaji huduma yake, kwa mujibu wa Meneja wa mchezaji huyo, Hanii Kessy.

**Ajibu ambaye alirejea Simba msimu huu akitokea Yanga, amekuwa katika wakati mgumu wa kupata namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza cha 'Wekundu wa Msimbazi' hao ambacho kimesheheni viungo wengi wanaowania nafasi moja.**

Hata hivyo, Meneja wake, Kessy amemtetea Ajibu akieleza kuwa kukosa namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza cha Simba kumetokana na changamoto mbalimbali alizokuwa akipitia msimu huu ikiwamo kuwa majeruhi pamoja na matatizo ya kifamilia ambayo yalimlazimu kuwa nje ya uwanja kwa muda.

"Ajibu ni mchezaji mwenye kipaji sana, na kilichomsababisha kutokupata nafasi mara kwa mara Simba ni kutokana na kuwa nje akiuguza majeraha na wakati mwingine matatizo ya kifamilia, alivyorejea akakuta tayari kocha ana timu yake ya ushindi, ambayo ilikuwa vigumu kuibadili, lakini hata hivyo amekuwa akipewa nafasi na kocha mpya [Sven Vandenbroeck]," alisema.

Alisema ligi itakaporejea hapatakuwa na mchezaji Simba wa kuweza kumweka Ajibu benchi na kwamba Sven amekuwa akimpa nafasi nyingi tu licha ya kwamba tayati timu hiyo ilishakuwa na kikosi chake cha ushindi.

Alisema kipaji alichonacho Ajibu ni cha kucheza soka nje ya nchi na jukumu hilo kwa sasa lipo mikononi mwa klabu yake kuamua kumruhusu ama la, kwa kuwa hawezi kulizungumzia hilo kutokana na bado ana mkataba na Simba.

"Hawezi tena kwenda Yanga hata Azam, kuna ofa nyingi tumezipata kutoka klabu za nje, lakini tunaheshimu mkataba wake, hivyo timu zinazomtaka tumekuwa tukizitaka kuwasiliana kwanza na Simba kwa kuwa bado wanamkataba naye," alisema.

Kabla ya kurejea Simba akitokea Yanga msimu huu, TP Mazembe ya DR Congo ilionyesha nia ya kumsajili, lakini kiungo huyo aliikataa ofa hiyo na kuamua kurejea klabu yake hiyo ya zamani ambapo amekutana na ushindani mkubwa wa namba unaomfanya mara nyingi kuanzia benchi.

Hata hivyo, licha ya Kessy kutokuwa tayari kutaja klabu zinazomhitaji Ajibu kwa sasa, kuna tetesi kuwa TP Mazembe ni miongoni mwa klabu ambazo zimeonyesha tena nia ya kurejea kuitafuta huduma ya kiungo mshambuliaji huyo kuelekea dirisha lijalo la usajili.

Tangu arejee Simba msimu huu Ajibu ameifungia bao moja pekee, alilitolifunga wakati timu hiyo hiyo ikiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania Januari 5, mwaka huu katika Uwanja wa Taifa.

Katika mechi hiyo ambayo Polisi Tanzania ilitangulia mbele kwa bao la Sixtus Sabilo huku John Bocco akiisawazishia Simba dakika ya 57, wakati mashabiki wakianza kutoka nje ya uwanja wakiamini mechi hiyo itamalizika kwa sare ya 1-1, Ajibu alibadili matokeo dakika ya 90 kwa kufunga bao la ushindi.

Akizungumzia nafasi anazopata Simba, chini ya Sven, Ajibu alisema: "Nimecheza mechi nyingi kuliko zile nilizokaa benchi tangu aje kocha huyu ndani ya Simba.

"Mwanangu aliumwa na kulazwa hospitali sikusafiri na timu nikawa namhangaikia yeye na hapo wenzangu wakaenda kwenye mechi dhidi ya Mtibwa Sugar na Lipuli kule Iringa.

"Inafahamika timu inayoshinda haibadilishwi ndiyo maana nikakosa nafasi, lakini tangu kocha huyu kaja nina nafasi,"

# Serikali yapokea maoni ligi kurejea

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI kiu ya mashabiki wa soka Tanzania ikiendelea kuwa ni lini Ligi Kuu itarejea tena baada ya kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyoitesa dunia, serikali imewataka kuvuta subra kwa kuwa tayari imepokea maoni mbalimbali kutoka kwa wadau wa soka.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Msemaji wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, ambapo alisema yeye pia ni mdau wa soka na anatamani kuona ligi hiyo hata leo ikirejea, lakini ni lazima serikali ijiridhishe kwanza kupitia kwa wataalamu wake mbalimbali kabla ya kuruhusu kurejea.

Hivi karibuni Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, alisema anafikiria kuruhusu ligi kurejea baada ya kusimama kwa muda na kwamba anachosubiri kwa sasa ni kupata ushauri kutoka kwa wataalamu wake, na baada ya kauli hiyo tayari serikali imefanya kikao cha pamoja na Bodi ya Ligi pamoja na Baraza la Michezo nchini kutathmini namna gani ligi itachezwa ikiwa ni pamoja na kupokea maoni kutoka kwa wadau wa soka.

Akizungumza kupitia kituo kimoja cha Redio cha jijini Dar es Salaam jana, Dk. Abbas, alisema serikali bado haijatoa uamuzi wa mwisho na wanachokifanya sasa ni kuangalia kamauamuzi huo utatolewa ligi ichezwe kwa namna gani kutokana na kuwapo kwa janga la corona.

"Kulikuwa na tathmini tu na kupokea maoni namna gani ligi ichezwe, kuna maoni ya kuchezwa kituo kimoja na yapo yanayotaka ligi ichezwe kama kawaida nyumbani na ugenini, pia wapo wanaosema ligi ichezwe na mashabiki lakini wakae mbalimbali, haya yote tumeyachukua na tunayafanyia kazi," alisema.

Alisema hayo yote yatapelekwa kwenye kamati kuu ambapo pia watashirikishwa wataalam wa afya pamoja na kamati ya wataalam wanaoishauri kamati kuu.

" Tunaendelea kupokea maoni lakini pia tunasubiri uamuzi wa mwisho wa serikali kuu ya kurejeshwa kwa michezo," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >